Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

REVISE AND ATTEMPT ALL THE EXERCISES

**USE THE SAMPLE** COMPOSITIONS TO DEVELOPE YOUR OWN

# Kusoma: Ufahamu

## Upembuzi wa ufahamu Maana ya ufahamu(meaning)

Ni makala(context) maalumu(specific) au kifungu maalumu cha habari ama taarifa ambayo hutolewa ili isomwe kwa makini kisha kuyajibu maswali yanayoulizwa kutokana na makala hayo.

## **Madhumuni ya ufahamu-the role**

Ni kupima uwezo wa msomaji katika kuelewa na kuyafahamu yaliyomo kwenye makala akitumia ujuzi wake wa lugha ili aweze kuyajibu maswali kwa usahihi, ufasaha na uzingatifu unaokusudiwa.

## Yaliyomo katika ufahamu

Kifungu cha ufahamu kina mambo na maarifa mengi sana yanayobidi kuzingatiwa wakati wowote kifungu hicho kinaposomwa. Mathalani, katika makala ya ufahamu kuna:

(i) Sentensi : Katika kila sentensi kuna wazo au dhana fulani muhimu inayohusiana na taarifa nzima ya habari katika kuendeleza maudhui ya taarifa hiyo.

(ii) Aya : Hiki ni kifungu kamili kilicho na wazo au tukio fulani maalum katika taarifa. Idadi za aya ndizo idadi za matukio katika taarifa. Kila aya ni mfululizo wa visa au vitushi vya taarifa-paragragh

(iii) Lugha : Katika lugha inayotumika kwenye taarifa ya ufahamu huwa na ufasaha, misemo, methali, misamiati maalum, nahau pamoja na mbinu au fani zote zinazotumika kuipamba na kuipanga taarifa.

(iv) Mantiki : Haya ni maarifa na fikra nzito ambazo huhitaji kuwaza na kuwazua kwa akili zilizomakinika ndipo msomaji awez kuyang'amua kwa kujiuliza maswali kadhaa k nini? (b) Maana yake nini Kwa nini? (d (e) Vipi? ( Wapi?-concept

(v) Wahusika: Hawa ni watu wanaotajwa kuhusika katika taarifa Huenda wahusika wakawa ni viumbe tu vya aina nyingine licha ya wanadamu. Lakini kujua na kuzingatia ni kuwa (a) Ni kina nani mhusika amehusika vipi Ametajwa vipi na kwa nini (d) Ametaja nini na kuhusika vipi? (e) Kila mhusika ana uhusiano gani na wenzake (f) Amehusu na kuhusika vipi? (g) Ni yupi mhusika au mtajwa mkuu

(vi) Kiini, dhamira, lengo(objective maudhui(themes):

Haya ndiyo mambo muhimu yaliyozua na kuzaa taarifa ya ufahamu. msomaji kusoma na kuelewa barabara

(a) Kiini cha habari au dhamira ama lengo kamili katika habari.

(b) Maudhui au mafunzo au matukio ya taarifa hii ni yapi

(vii) Kichwa au Anwani : kuisoma na kuielewa habari barabara ni rahisi msomaji kupata kichwa au anwani hata kama taarifa yenyewe haikuwa na kichwa wazo kuu au dhana inayojitokeza na kupewa uzito katika taarifa kuwa kichwa au anwani



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

(viii) Mazingatio :Mwanafunzi au msomaji akisoma kwa kuyazingatia mambo hayo yote.ni rahisi kukabili na kuyajibu maswali yoyote yatakayoulizwa kutokana na taarifa yenyewe.-considerations

(ix) Maswali : Baada ya kusoma taarifa ya ufahamu, msomaji hulazimika kuyajibu maswali yaulizwayo. Maswali hayo ya ufahamu yanahusu:

(a) Kuandika au kuchagua kichwa mwafaka kulingana na taarifa
(b) Kueleza au kutambua maana ya baadhi ya maneno jinsi yalivyotumika katika habari.
(c) Maswali ya mantiki yanayohitaji kuwaza, kufikiri na kuchambua kiini cha mambo.
(d) Maswali rahisi ya moja kwa moja kuhusu wahusika, matukio na yaliyomo katika taarifa.
(e) Maana na matum z ya methali au miserr: iliyotumika kwen.e habari.
(f) Wahusika au wc:. waliotajwa, maner: yao na kuhusikc kwao katika k s: kilichosimuliwa.
(g) Kiini au maudhui yc baadhi ya matuk: fulani fulani.

## Jinsi ya kusoma taarifa ya ufahamu

Kwanza usiisome taarifa ya ufahamu kwc papara au kwa akili ambazo hazijatulia Hii ndiyo sababu utakuta ukiambiwc isome taarifa ifuatayo kwa makini kishc uyajibu maswali. Lazima uwe umemakinikc unapousoma ufahamu. Hata hivyo, hatuc muhimu za kuisoma taarifa ya ufaham. ni hizi tatu:

### Hatua(step) ya kwanza

Shika kalamu na uanze kuisoma taarifa kwc utulivu mfululizo mwanzo hadi mwisho ili angalau uelewe habari hiyo inazungumzic mambo gani, kisa gani au tukio gani kwc jumla. Kinachohitaji hapa ni kupata fununu kuhusu kiini cha habari kama juu ya Njaa. Elimu, Maradhi, Michezo, Usafi, Mafuriko. Safari, Adabu, Kilimo au vyovyote vile.

### Hatua ya pili

Baada ya kuisoma taarifa hiyo kwc mfululizo, anza kuisoma tena kwa mara ya pili huku ukiyazingatia mambo muhimu au matukio makuu yanayojitokeza na kutajwa katika habari. Kila unapoyagundua mambo hayo muhimu yanayochukua uzito katika habari, uyapige mistari ili yaonekane dhahiri kwani huenda yakakusaidia katika kupata majibu kutokana na maswali yaulizwayo.

### Hatua ya tatu

da ya kuisoma taarifa mfululizo, me tena kwa kuzingatia mambo imu yaliyotokeza au kutajwa kwa o kulingana na kiini cha habari, sasa, irza kusoma swali moja moja huku j<Jrejelea taarifa ili uone kuwa swali . olisoma laweza kuwa limedondolewa kitoka kipengele kipi cha habari. Fanya - - jo kwa kila swali linalohitaji kurejelewa **<.'.oka** kwenye taarifa. Kumbuka maswali "engine ni dhahiri na ya moja kwa moja, -.-eweka bila kuhitaji marejeleo ya —nrifa. Mtindo huu wa kulisoma swali ■ xxu ukiirejelea taarifa hukupa hakika ya <_;ata jibu sahihi lililodhamiriwa tu kati ya ~ ajibu yoyote yaliyotolewa kukubabaisha.

## Misamiati katika ufahamu

Msamiati au misamiati ni jumla ya ~aneno yoyote yanayotumiwa katika jjgha. Lakini katika taarifa ya ufahamu, -samiati au misamiati ni maneno maalumu ,aliyoteuliwa rasmi kutumiwa katika « fungu cha habari iliyotolewa. Huwa ni -aalumu au rasmi kwa sababu neno la zwaida linaweza kutumiwa katika habari i kuleta maana mahususi iliyodhamiriwa :j kwa mujibu wa habari hiyo. Aghalabu -nambo hayo hutokea kuhusu vitawe au maneno yenye maana zaidi ya moja. <wa hivyo, ukiambiwa ueleze maana ya msamiati fulani uliotumika katika taarifa, usisumbuke wala kupoteza wakati kutaja au kutoa maana ambayo hayalingani na dhamira ya habari. Mathalani, katika taarifa, kifungu kinasema, "Haikuwa ada ya wanakijiji kuamka alfajiri na mapema kwenda makondeni. Walizama katika uzembe wa kulala fofofo hadi jua la utosini..."

Hapa ada si malipo wala walizama si kwamba waliingia majini. Kwa mujibu wa kifungu, ada hapa ni tabia, mazoea, desturi nalo neno walizama maana yake ni walikwama au walijifunga.

Hiyo ndiyo sababu unaambiwa, "Eleza msamiati fulani jinsi ulivyotumika katika habari ..."



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

KUMBUKA: Ili kupata maana sahihi ya msamiati jinsi ulivyotumika katika taarifa, uisome sentensi nzima au aya nzima iliyoshikamana na msamiati wenyewe ndipo uuchambue na kuutambua una maana gani kulingana na muktadha wa yale yanayotajwa hapo.

## Taswira ya ufahamu

Soma vifungu vifuatavyo vya ufahamu kwa kuzingatia maelezo na maelekezo uliyopewa hapo awali ili ujibu maswali.

### Kifungu cha kwanza

Soma kifungu kifuatachao, kisha ujibu **maswali 1-10**

Wanafunzi wa darasa la nane wa Shule za msingi za Bagamoyo na Kigoma walikutana katika ukumbi wa shule ya Kigoma. Maandalizi ya mjadala uliokuwa umesubiriwa kwa hamu na pashau yalikuwa yamekamilika. Baada ya wimbo wa taifa kuchezwa, mwenyekiti alianza, "Mtoto ana haki mzomzo. Iwapo jambo hili halitapigwa darubini, basi huenda jamii ikapoteza warithi wake. Naomba washiriki wajibwage uwanjani ili tujadili suala hili."

Ghafla kama aliyedungwa sindano ya maneno, Menomeno alisafisha koo na kuanza, " Asante sana bwana mwenyekiti, mtoto ana haki ya kukidhiwa na kulelewa barabara. Anahitaji kuchanjwa, kupewa viinilishe ili asivie au kuugua maradhi kama utapiamlo na nyongea."

"Mlo pekee si hakikisho la rai aula ya mtoto." Jichopevu alimchachawiza Menomeno, "Mtoto anastahiki kupewa ushaurinasaha ama elimu ya dunia. Elimu hii itamwepusha dhidi ya vishawishi vya uraibu wa mihadarati ambayo huathiri siha ya mraibu kwa kusababisha magonjwa



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

kama saratani ya mapafu na midomo, shinikizo la damu, wazimu na mengi mengineyo. Aidha afahamishwe kuwa ni kinyume cha maadili kwa mtoto kushiriki katika ngono ambayo itamletea balaa na belua. Madhara makuu ni ukongo wa zinaa kama UKIMWI, kaswende na kisonono. Fauka ya hayo, anaweza kupata himila. Je, mtoto atawezaje kumlea mtoto licha ya kumkimu? Vile vile, mwana anapougua hana budi kupewa matibabu ya dharura."

"Kongole Jichopevu," Kidete akasimama kwa hoja ya nidhamu na kuendelea. "Bwana mwenyekiti mavazi ni faradhi kwa mtoto. Si vyema kumvisha mtoto mavulia daima. "Aaa!!" umayamaya wa wanafunzi ukanong'ona. Ni hati..." "Mavulia! Mavulia!" Dakia alimdakiza. "Bwana mwenyekiti ni makosa makubwa kwa Kidete kupotosha umma. Sioni tatizo lolote kwa mnuna wangu kuvaa nguo zangu ambazo zinanibana. Mbali na hayo, yapo mavulia mazuri kuliko hata nguo mpya zinunuliwazo madukani."

"Kunradhi Dakia pamoja na hadhira. Nilidhamiria kutaja mararumararu au mavazi yaliyochanika chanechane tamthili ya majani ya migomba. Hata hivyo, si vyema kwa watoto kupuuza mavulia kwa kuwaona wenzao takriban wote wakiwa na mavazi mapya. Huenda wazazi wao hawana uwezo wa kumudu gharama ya mavazi mapya. Wakumbuke kuwa, afadhali dooteni kama ambari kutanda."

"Mtoto anafaa kuishi katika mazingira ya kuvutia. Aishi katika maskani ya kuvutia na nadhifu ili kumwepusha na maradhi kama malaria ambayo husababishwa na mbu. Pia nyumba ipigwe deki au kufagiliwa ili kufukuzilia mbali vimelea kama tekenya au funza. Aidha jamii sharti imfunze kuyatunza. Ni vyema jamaa kuhakikisha mtoto anaishi katika mazingira yenye amani na utangamano. Aishi kwa kuonyeshwa kuthamini ubinadamu. Asipigwe, kudhalilishwa, kufanyishwa kazi za sulubu na shokoa, kuajiriwa, kuozwa kwa lazima ama kukeketwa na kubaguliwa kwa misingi ya jinsia." Sadfa alifafanua.

"Ninamwunga mkono Sadfa Bashasha alisema, "Mtoto apewe muda wa kucheza. Afunzwe kuheshimu kuwajibika katika dhima za kiwango chake. Yafaa ahakikishiwe usalama wala asiishi roho mkononi."

"Samahani, bwana mwenyek: akasihi Saad, "Namwomba Bashasha aelez; kinagaubaga namna ya kumwepus- : mtoto hofu ya ulimwengu wa major;; kama milipuko ya mabomu na magrure: moto, zilizala, gharika, maporomoko = z ardhi, uvamizi na njaa."

"Shukrani. Elimu ya mtoto itakamilika iwa--: atafunzwa misingi ya dini itakayomwezes-: kuishi kwa uadilifu na kumhami na uwez; wa kustahimili masaibu ambayo yak: juu ya uwezo wa mwanadamu. Elirr. itakayowafunza kujali maslahi ya wengin= kuwasikiliza, kuwavumilia na kuwapendc Jambo adhimu zaidi ni kumwezesha mwan: kukua kwa kujitegemea na kutegemewa nc wengine."

Pande zote mbili ziliafikiana kutunzc haki za binadamu. Aidha serikali nc jamii husika ina wajibu mkubwa wa kumlinda mtoto bila ubaguzi. Majadilianc yaliyopamba moto yalifikia hatima nc makundi yote kupeana mikono ya tahania.

## Maswali

1. Kwa mujibu wa kifungu, shule za Kigoma na Bagamoyo zilijumuika ili

   A. kushiriki katika mdahalo kuhusu asili ya haki za watoto na kuzitatua.
   B. kubadilishana mawazo kuhusu chanzo cha dhuluma za watoto.
   C. kujadili na kupiga darubini hatari ya jamii kupoteza warithi.
   D. kubadilishana mawazo juu ya changamoto zinazowakabili wana kielimu.

2. Si kauli ya Menomeno kuwa
   A. ni haki ya mtoto kuengaengwa.
   B. mtoto ana haki ya kupewa matilaba.
   C. mtoto hana budi kupewa lishe bora.
   D. mtoto hana budi kupewa huduma za matibabu.

3. Maoni ya Jichopevu ni kuwa, Elimu ya Dunia
   A. humwepushia mtoto maradhi ya UKIMWI, mihadarati na himila.
   B. humsaidia mtoto kukabiliana na ushawishi potovu wa marika.
   C. humwepushia shinikizo la damu, mihadarati, ngono na UKIMWI.
   D. humsadia kujua UKIMWI, ngono na dawa za kulevya.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

4. Neno rai kwa mujibu wa kifungu Una maana ipi?
   A. Maoni B. Bembeleza
   C. Siha D. Ushauri
5. Kulingana na ufahamu ni ipi maana ya mbali na hayo ?
   A. Maadamu B. Fauka ya
   C. Mradi D. Madhali
6. Wakumbuke kuwa,'afadhali dooteni kama ambari kutanda.' Maneno haya yana maana kuwa .
   A. ni bora kupata mavazi makuukuu unayoweza kumudu.
   B. ni heri mavazi ya kifahari iwapo utaweza kumudu.
   C. wazazi wetu hawana uwezo wa kumudu mavazi.
   D. kila mzazi hana budi kujitahidi kuwanunulia wana mavazi.
7. Kifungu kinatueleza kwamba ni jukumu la .
   A. serikali kuhakisha kuwa watoto wanaishi kwa amani.
   B. jamii kuhakikisha kuwa wana wamelelewa katika mazingira ya amani.
   C. jamaa kuhakikisha kuwa watoto wanaishi katika mazingira ya amani na utengano.
   D. jamii kuhakikisha kuwa udhalilishaji wa jinsia umedumishwa.
8. Wajibu wa watoto ni
   A. kucheza, kuheshimu na kuwajibika.
   B. kuheshimu, kuwajibika na kutekeleza wajibu wao.
   C. kuhakikisha usalama wake mwenyewe.
   D. kutunzwa, kucheza na kudumisha usafi.
9. Mtoto anaweza kuondolewa hofu ya majanga kutokana na
   A. kupata haki zake za kimsingi na kupewa elimu ya dini.
   B. kumwelimisha hadi chuo kikuu na kumpa elimu ya dini.
   C. kupewa elimu ya dini, kufunzwa uadilifu na kuthamini ubinadamu.
   D. kupewa elimu ya dini, kufunzwa kushtaki maonevu, kupewa haki.
10. Katika aya ya mwisho, mwandishi anasema kuwa
   A. ni jukumu la jamaa na serikali kuhakikisha wana wanatuzwa.
   B. ni wajibu wa washikadau wote kuhakikisha kuwa, wana wana usawa na kulindwa.
   C. ni wajibu wa serikali na jamii husika kuhakikisha wana wanatuzwa.
   D. ni jukumu la wadau wote kuhakikishia wana udhalilishaji wa jinsia.

## Kifungu cha pili

Soma habari hii kwa makini kisha ujibu maswali **1-10**

Hauchi hauchi unakucha. Hatimaye ziara tuliyoisubiri kwa hamu na pashau ilifika. Siku ya safari tuliyozawadiwa na rais kwa ushindi wetu iliwadia. Usiku wa kuamkia siku hii sikupata hata lepe la usingizi. Matarajio makuu yalinifanya kudamka alfajiri na mapema hata kabla ya jogoo la kwanza. Hata kiamshakinywa sikudiriki kukila vizuri kutokana na shauku iliyonikumbatia.
Nilitembea kutoka pembe moja ya sebule hadi nyingine kama mtu anayemtarajia mgeni ambaye amechelewa. Hatimaye, niliamua kulifungua sanduku langu la usafiri na kuanza kulikagua tena huku nikihakikisha kwamba chochote nilichohitaji kwa safari kilikuwemo.

Nilikumbuka ushauri wa mwalimu wetu Bwana Tembo. Mwalimu Tembo alikuwa ametutahadharisha tusibebe vitu vyenye makali kama vile vyembe au visu. Hakusahau kutukumbusha tuhakikishe kuwa mizigo yetu haizidishi uzani unaokubaliwa katika ndege. Mimi binafsi nilikuwa nimeupima uzani wa sanduku langu na kuhakikisha kwamba lina uzani ufaao. Kadhalika, nilikuwa nimezihifadhi stakabadhi zote za usafiri ndani ya mkoba mdogo wa mkononi.

Hata basi lilipowasili kwenye lango letu kutupeleka kwenye uwanja wa ndege, sikuacha kumshukuru Mungu kwa ushindi tuliopata katika mashindano ya kitaifa ya michezo ya kuigiza. Kwa kweli ushindi huu hatukuupata tu, tulikuwa tumechanika kwenye mpini. Lililonipa fahari kuu ni kwamba mimi ndimi niliyebuni mchezo huu chini ya uelekezi wa Bwana Tembo. Lililomvutia rais zaidi katika mchezo huo ni mada yake, pamoja na yaliyomo. Mchezo wetu ulipinga ufisadi na ukabila. Mhusika mkuu wa mchezo huu alikuwa waziri ambaye aliongozwa na tamaa kuiba mali ya umma. Mwishoni mwa mchezo , waziri huyu alipata adhabu ambayo ilimfanya kubadilika.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Basi baada ya rais kuutazama mchezo huu kwenye ikulu, alitutunukia safari ya ng'ambo.

Tuliwasili kwenye uwanja wa ndege saa mbili asubuhi, kila mmoja akiwa hoi kwa bashasha. Ilikuwa kioja kwa wengi kuona uwanja uliorembwa kwa ndege za kila aina na kimo. Wengi wetu tulikuwa tunaziona ndege zikiwa juu angani, hili la kuweza kuingia ndani, sikwambii kuiabiria hatukuwahi kuliotea! Hata tulipoagizw; kupitia kwenye mtambo fulani kukaguliwc sikumbuki yaliyojiri kwani macho yc mawazo yangu yalikuwa mbali kule-e-e-.

Tulipoingia ndani ya ndege miship: yangu iliganda kwa mshangao. Kumbe ndani ya ndege huwa na runingc Nilimwomba Bwana Tembo niketi kwenye kiti ambacho kilikuwa na runinga yenye picha ya mtangazaji maarufu nchini. Hate hivyo, Bwana Tembo alinifahamisha kwambc hicho ni kitengo cha wasafiri wa hadhi yc juu zaidi, akaniambia kwamba hata sisi tulikuwa tumetengewa mahali petu. Safari iliiva tukajifunga mikanda ya usalama na ndege kuanza safari kwenye kibarabara. Moyo wangu uliingiwa na shaka, nikajiuliza, "Kwani ndege huendeshwa kama gari?" Lakini ghafla nilisikia mngurumo usio wa kawaida na kuona ndege imetandaza mbawa na kuruka angani kama nyuni. Hapo ndipo nilijua .kwamba safari ya ng'ambo kweli imeanza. Niliyaelekeza macho kwenye kidirisha kilichokuwa ubavuni mwangu na kuanza kuyafurahia mandhari kwenye vilele vya mawingu. Chambilecho wahenga, kutembea kwingi kuona mengi.

## Maswali

1. Msimulizi aliamka mapema kwa sababu .
   A. walikuwa wametunikiwa safari na rais.
   B. alikuwa na hamu kuu ya kusafiri ng'ambo.
   C. alikuwa na tumaini kuu la kuona watakaoenda ng'ambo.
   D. walikuwa wameambulia ushindi kwa Rais.
2. Aya ya pili imebainisha kwamba msimulizi .
   A. ni mwenye hakika.
   B. anatambua maagizo ya safarini.
   C. ni mwenye makini
   D. anaheshimu hali ya mwalimu.

Kulingana na aya ya tatu, .

A. msimulizi ndiye aliyechangia zaidi katika ushindi wao.

B. ushindi katika ngazi ya kitaifa ulihusiana na ukabila.

C. mwongozo wa Bwana Tembo ndio ulioipa timu hii ushindi wa kipekee.

D. uigizaji wa wanafunzi ulilingana na jinsi walivyobuni.

Chagua jibu sahihi kwa mujibu wa kifungu.

A. Mchezo ulishinda kwa sababu ulikashifu maovu.

B. Rais alipendezwa na mchezo kwa sababu ulihimiza maadili.

C. Mada ya kushinda ilichochewa na matendo ya mhusika mkuu.

D. Kuteseka kwa waziri kulitokana na kudhulumiwa mchezoni.

Ni dhahiri kwamba, . .

A. baadhi ya wanafunzi hawakuwa na habari kuhusu ndege zitakapoabiriwa.

B. ilikuwa mara ya kwanza kwa wanafunzi kuona ndege za aina hii.

C. walikuwa wamejawanamshangao kuhusu ndege kuliko awali.

D. idadi kubwa ya wanafunzi haikuwa na matumaini ya kuabiri ndege.

Msimulizi .

A. hakuutambua mtambo kwa vile alikuwa ameduwaa.

B. hakushuhudia kuchunguzwa kwani hakuwa makini.

C. hakuona yaliyotokea kutokana na hamu aliyokuwa nayo.

D. hakuwazia yaliyotendwa kulingana na matarajio yaliyokuwepo.

Kulingana na kifungu, .

A. msimulizi alifurahishwa na kuwepo kwa mtangazaji kwenye runinga.

B. wanafunzi hawakuruhusiwa kuketi pamoja na wasafiri wengine.

C. nafasi za kuketi kwenye ndege hupangwa kulingana na hadhi ya wasafiri.

D. vyombo vya habari hutumiwa na wasafiri wachache katika ndege.

8. Kauli "Kwani ndege huendeshwa kama gari?" inaonyesha kuwa

   A. msemaji hajawahi kuona rubani akiendesha ndege.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

B. mzungumzaji anaona kwa mara ya kwanza ndege ikianza safari.
C. msimulizi hakuweza kuwaza kuwa ndege huonekana barabarani.
D. mnenaji anatambua ghafla kuwa ndege hupitia barabarani kabla ya kunguruma.

9. Tulikuwa tumechanika kwenye mpini,' ina maana kuwa
A. Ushindi wao ulitokana na matumizi ya mazoezi yaliyopatikana mashindanoni.
B. Kufaulu kwao kulitokana na kujitolea kwao kujiimarisha.
C. Kutunukiwa kwao kulitokana na kujaribu kwao kufuata maelekezo.
D. Umaarufu wao ulitokana na uzingatiaji wa mada iliyochaguliwa michezoni.

10. Maana ya, 'Kila mmoja akiwa hoi kwa bashasha,' ni kwamba
A. wote walikuwa na furaha kupita kiasi.
B. wote walikuwa na matumaini yaliyozidi.
C. wote walikuwa na mshangao uliowachangamsha.
D. wote walikuwa na matarajio ya kupindukia.

## Kifungu cha tatu

**Soma makala haya kisha ujibu maswali 1-10**

Usafiri unaweza kuelezwa kuwa ni hali ya safari ya chombo cha kusafiri au shughuli ya kusafirisha watu na mizigo. Ili kufanikisha usafiri, lazima pawepo chombo. Mti hauendi ila kwa nyenzo. Baadhi ya vyombo vya usafiri ni: ndege, meli, garimoshi, magari, ngamia, punda, baiskeli na hata pikipiki bila kusahau usafiri wa miguu. Chombo cha usafiri hutegemea uwezo wa mtu kiuchumi au masafa ya safari. Hebu tuchunguze kwa kina usafiri wa pikipiki ambao umeathiri jamii ya sasa sana.

Usafiri wa pikipiki almaarufu 'bodaboda' umeleta mapinduzi makubwa katika sekta ya usafiri wa umma.

Awali, pikipiki zilimilikiwa na wachache waliokuwa na uwezo mkubwa kiuchumi. Kadhalika, pikipiki zilitumiwa ama katika usafiri wa mtu binafsi au mashindano ya riadha. Hii leo, sekta ya usafiri imetwaa sura mpya kutokana na matumizi anuwai ya pikipiki. Kinyume na awali ambapo watu binafsi huenda walitumia pikipiki katika shughuli za kikawaida siku hizi pikipiki huwasafirisha watu na bidhaa kwa malipo. Ni kawaida kuwapata watu wawili au hata zaidi wakiabiri pikipiki moja.

Pikipiki zimerahisisha usafiri hasa katika sehemu ambazo hazifikiki kwa kukosekana au kuharibika kwa barabara. Aidha, pikipiki huwaokolea muda wasafiri. Badala ya mtu kutembea hadi kituo cha magari, anaweza kumpigia simu mwendeshaji pikipiki akamchukua hapohapo nyumbani au popote alipo. Hili linarahisisha shughuli za kuzalisha mali. Kadhalika, usafiri huu, umesaidia kubuni nafasi za kazi. Wapo raia ambao wameweza kujiajiri na kuwaajiri wengine kuwaendeshea biashara hii. Matokeo ni kwamba, idadi ya wanajamii ambao wangeshiriki uhalifu ili kujipatia riz« imepungua.

Juu ya hayo, usafiri huu umechang : katika kuimarisha mshikamano wa kijam Wenye pikipiki hizi wameungana kuunc: vyama vya ushirika. Pamoja na vyamc hivi kuwaunganisha, wanachama huwez: kupata mikopo ya kupanulia biasharc au hata kuanzisha biashara nyingine Vyama hivi pia hutoa ushauri kw; wawekezaji wachanga wanaojiunga nc sekta hii. Kadhalika, kwa vile wenye pikipik hizi wanajulikana, ni rahisi kwa maafisc wa usalama kudhibiti uhalifu unaowezc kuendelezwa na waendeshaji pikipiki.

Hakuna masika yasiyokuwa na mbi. Usafiri wa pikipiki unaandamana nc changamoto nyingi. Uendeshaji pikipik kiholela umesababisha ajali, ulemavu nc vifo. Kadhalika kelele nyingi huhinikizwc katika sehemu ambapo pikipiki hutumiwa. Hili huvuruga shughuli nyingine kamc vile masomo shuleni na ibada maabadini. Isitoshe, msongamano wa pikipiki katika maegesho mijini na vijijini huwatatiza. si wapita njia tu, bali pia waendeshaji magari. Si ajabu kupata hata waendeshaji magari wakitingwa na pikipiki kiasi cha kusababisha ajali.

Usafiri wa pikipiki umetumiwa kama nyenzo ya kuendeshea uhalifu. Mathalan, waendeshaji wa pikipiki wamejigeuza wamiliki wa maegesho na kuwanyima wengine uhuru wa kuyatumia. Hili huzua kutoelewana na hata mapigano. Pia pikipiki hutumiwa kuendeleza wizi, utekaji nyara na ulipuaji wa binadamu na majengo kwa guruneti au mabomu. Kwa sababu ya ule wepesi wa pikipiki , ni rahisi kwa mhalifu kufyatua risasi au kutupa kilipuzi chake na kujiendea. Waendeshaji pikipiki wengine



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

huwapora abiria wao na hata kuwanyanyasa kimapenzi.

Ili kufanikisha aina hii ya usafiri, jamii haina budi kukabiliana na matatizo latokea. Vilevile, abiria sharti wawajibike <upinga ubebaji wa abiria na mizigo ngi kupindukia. Kadhalika, wana haki ya kumwonya mwendeshaji dhidi kuendesha kwa kasi isiyokubalika. **cdereva nao wapewe mafunzo kuhusu .^-reshaji ufaao, na kupewa kibali cha -e-ideshea wanapohitimu. Sheria za ii-abarani zizingatiwe na watumiaji wote -z barabara. Wanaokiuka sheria hizi -atiwe mbaroni na kuchukuliwa hatua zfaazo.

## Maswali

Usafiri wa pikipiki umesababisha mabadiliko kwa vile .

A. zamani kinyume na siku hizi, pikipiki zilitumiwa sana na watu wenye vyeo vikubwa.

B. kinyume na siku hizi, pikipiki zilitumiwa kuendeshea mashindano nyanjani.

C. tofauti na zamani, siku hizi pikipiki zina matumizi mbalimbali.

D. awali, kinyume na siku hizi, pikipiki zilikuwa na matumizi ya kipekee.

Aya ya pili imebainisha kwamba

A. pikipiki hutumiwa kama njia ya kufanikisha biashara. 3. watu waliendesha pikipiki zilizolipiwa.

C. watu walitumia pikipiki katika mahali pa kuchezea.

D. pikipiki huendeshwa kwa zaidi ya mtu mmoja.

Wasafiri wamefaidika kivipi?

A. Wanaabiria popote, wanarahisishiwa utendakazi.

B. Wanafika haraka, wamepunguziwa uhalifu.

C. Hawachoki kutembea, wanaajiriwa nyumbani.

D. Hawakosi kupita, wanapata huduma hapohapo.

C. Watu huzoana wanaponyimwa haki.

D. Abiria hupoteza mali yao wanapobebwa.

yanaoikumba. Abiria anastahili kuvaa mavazi yanayomkinga iwapo ajali

Ni jibu lipi lisilo sahihi kwa mujibu wa aya ya tatu?

A. Pikipiki huweza kufanikiwa pale ambapo magari hayafanikiwi.

B. Kusafiri huwa kwepesi kwa pikipiki pale pasipokuwa na gari.

C. Usafiri wa pikipiki huinua uchumi wa nchi.

D. Abiria humfikia mwenye pikipiki kwa urahisi.

Kulingana na aya ya nne, .

A. madereva wameungana na kusikilizana kuhusu biashara zao.

B. wafanyabiashara wanapata maarifa ya kuendeshea kazi zao.

C. wanajamii huwa na hazina ya kuanzishia miradi.

D. washiriki watafanya maamuzi na kujinufaisha kwa njia nyingi.

Imebainika kwamba .

A. watu wanaposhiriki kazi pamoja hupunguza uhalifu.

B. usalama huenezwa kwa watu wanaojuliana hali.

C. uovu katika jamii huzidishwa na watu kutofahamiana.

D. maafisa wanapofahamishwa nyendo za waendeshaji huimarisha utulivu.

7\. Uendeshaji pikipiki kiholela husababisha .

A. kutatizwa kwa usafiri, kudhoofika kwa mwili.

B. kuzorota kwa masomo na kelele kwenye maeneo.

C. kupoteza uhai, kuleta ajali garini.

D. kurundikana maegeshoni, kuwazuia walio njiani.

Ni jibu lipi sahihi kwa mujibu wa aya ya sita?

A. Wenye pikipiki hunyakua wanapoegesha.

B. Pikipiki huwaua watu inapoharibu majengo.

9\. Jibu lipi ni sahihi kulingana na aya ya mwisho ?

A. Madereva wanastahili kuhimiza kuzingatia sheria barabarani.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

B. Idadi ya mizigo ikizidi abiria, ajali itatokea.
C. Abiria wanahimizwa kudhibiti mwenendo wa dereva.
D. Kibali cha kuendeshea kitazuia kuvunja sheria.

10. Maana ya 'almaarufu' ni nini?
  A. Inayofanana na.
  B. Inayojulikana kama.
  C. Inayoendelezwa na.
  D. Inayotangazwa kama.

## Kifungu cha nne

Soma **taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali** niliguria yafuatayo 1-10.

Bwana Maisha alitokea kuwa maarufu sana pale mtaani Sipati. Umaarufu wake ulichochewa na kuvumishwa na kazi nzuri alizozifanyatena kwa kujitumia na kujitolea mno. Wazazi wengi pamwe na wenyeji kwa jumla walimchukulia kama kielelezo chema kwa wana wao na watu wazima pia. Akawa ndiye mtu wa kupigiwa mfano mara kwa mara. Lakini Bwana Maisha ni nani hasa? Tulia ufunuliwe kurasa za maisha ya bwana huyu.

"Mimi Bwana Maisha niliwahi kutumbukia katika kilindi cha ulevi nisijue jinsi ya kuogelea hadi ufuoni kujisalimisha nafsi yangu. Huu ulikuwa wakati wautomvu wa maisha yangu. Sikuweza kupambanua mbivu na mbichi. Mathalan nilikuwa tu bendera, nikifuata rubaa bila kuhoji nilikoelekezwa. Kwa takriban miongo miwili nikawa ni mimi na ugimbi na ugimbi na mimi. Sikulipata jina la Mwenyekiti wa waraibu hivi hivi tu; nilishastahili kwani sikuwa nambari mbili kwa yeyote yule.

Wakati wote huo nilikuwa na kis~ — cha kupata kazi hata bila ya kutaraz: Taaluma yangu ya ualimu ilinifanya kupc:: ajira katika shule za umma na hate :: kibinafsi. Sikitiko ni kwamba, mahudh.-: yangu kazini yalikuwa mabaya - : nilipopata mshahara. Aliyenite-: angenipata kwa akina mama pir>: Uhusiano wangu na watu wengine uka*c wa kubahatisha tu isipokuwa ware:. wenzangu. Niliwadhulumu wanafi.-; wengi walionitegemea kuwafunza b e hata ya kujali.

Nilizaliwa yapata miaka thelath -na mitatu iliyopita nikiwa mwana wa tc:. katika ahali ya wana wanne. Shinikizo : marafiki zilisababisha kutumbukia ulev-kichwa na kiwiliwili ingawa kwetu hakir: mtu mwengine aliyeshiriki ulevi wa air; yoyote ile.

Ujanani mwangu, nilishawishi-: kuhepa shuleni kuitika mwito wa pomzi Ya kwamba nilikuwa wembe masomc-isingekuwa ngao ya kunikinga dhic ya kutemwa kutoka shule hii wala :.e nyingine. Tabia zangu zilinuka karr: pombe zilizonitawala.

Nasaha za wengi walionithami-ziligonga mwamba. Niliziba masikio kwc nta na zege. Nisikie nini wala nimsikie nani? Wa kwangu walikuwa tu walev wenzangu tuliolandana kama sahani nc kawa. Nilihitimisha masomo ya upili baadc ya kusomea katika shule nne tofauti. Hali yangu ilikuwa mbaya. Lichc ya haya yote, niliweza kujiunga na chuc kikuu. Nilihitimisha masomo na kupatc shahada ya ualimu. Muda si muda. nilipata kazi katika shule mojawapo ya umma. Huko shuleni hakukuniweka. Ulevi usingeniruhusu kuendelea na kazi.

Nilipata kazi nyingine. Na kamc ilivyokuwa ada yangu, pindi mshahara ulipoingia kibindoni, aliyetamani maisha yangu.

Nilipelekwa katika kituo cha .-ekebishaji tabia na msamaria mwema uyeniokota barabarani nikiwa chakari. -uko ndiko nilikoweza kupata usaidizi na «jamua kumtupa jongoo na mti wake, -ya yangu ilikuwa imezorota ikabadilika a kuichukia **pombe** upeo wa chuki. Yakini **Dombe** haina manufaa bali ni sumu iuayo Dolepole. Enyi vijana nawaomba kamwe ■nsijaribu kuionja pombe. Mkondo wa Dombe ni hatari. Jihadhari kabla ya hatari.

## Maswali

1. Ni bay ana kwamba .
  A. bwana Maisha ni mchochezi pale mtaani.
  B. umaarufu wa bwana Maisha. umetokana na alivyokunywa pombe.
  C. bwana Maisha aliyafuja maisha ya kisogoni.
  D. bwana maisha ni mtovu wa maadili.
2. "Niliwahi kutumbukia katika kilindi cha ulevi..." Hii inamaanisha kuwa:
  A. msemaji aliteleza na kuanguka katika kidimbwi kilichojaa pombe.
  B. msemaji aliingilia ulevi bila kipimo.
  C. ulevi wa msemaji ulimlazimisha hadi ndani ya kilindi.
  D. msemaji alikuwa mlevi mashuhuri ambaye hangewezwa na pombe
3. Bwana Maisha .
  A. alianza kushiriki ulevi alipohitimisha masomo ya shule ya msingi.
  B. aliwadharau wote wasiolewa kama yeye.
  C. alithaminiwa kwa jinsi alivyotekeleza wajibu wake.
  D. alilewa na kutoweza kutofautisha matunda mabivu na mabichi.
4. Kauli '...nikifuata rubaa bila kuhoji nilikoelekezwa,' ina maana gani?
  A. Nilipenda kuogelea kutoka kilindini hadi ufuoni.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

B. Sikupenda kuulizwa ulizwa maswali ovyo.
C. Kila nilipoenda kuogelea daima nilijipata nikilewa
D. Niliandamana na wenzangu bila kudadisi walikonipeleka.

5. Ni kweli kwamba
   A. jina la mwenyekiti ni lakabu.
   B. kura zilipopigwa bwana maisha ndiye aliyeibuka kuwa mbele.
   C. msemaji alipiga lami kwa muda pindi alipofuzu chuoni.
   D. msemaji alipata ajira katika shule mbili kwa wakati mmoja

6. Kilichosababisha bwana Maisha kupigwa kalamu si .
   A. kuwafaa waraibu wenzake walipomwomba msaada.
   B. kuwadhulumu wazazi
   C. kuwatumbukiza marafiki maarufu katika ulevi.
   D. kuambaa kazi alipopata mshahara.

7. Kwa mujibu wa kifungu ni kweli kusema:
   A. Msemaji aliponea kufukuzwa shuleni kwa vile alivyokuwa mwerevu masomoni.
   B. Msemaji ametumia tembo kwa karibu miaka ishirini.
   C. Masikio ya msemaji yalikuwa radhi kusikia ushauri wa waenzake.
   D. Kujiunga na chuo kikuu kulimzoa msemaji kutoka katika ulevi.

8. Maana ya 'kutarazaki' katika taarifa ni .
   A. kukosa stakabadhi maalumu
   B. kubahatika kazi
   C. kushughulika
   D. kutabaradi



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

9. Ni yakini kwamba watu waliohusika katika kuathiri maisha ya msemaji si pamoja na .

A. marafiki wa utotoni
B. mama pima
C. msamaria mwema
D. wenyeji wote wa mtaani Sipati

10. Methali inayoweza kufafanuliwa na aya ya mwisho ni lipi?

A. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji
B. Cha mlevi huliwa na mgema
C. Aliyeonja asali huchonga mzinga.
D. Kutangulia kwenye baa si kutangulia kulewa.

## Kifungu cha tano

Soma **taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo 1-10**

Mojawapo ya malengo ya milenia ni kuondoa umaskini katika jamii. Juhudi kabambe zinahitaji kufanywa ili kuafikia lengo la jamii. Kati ya juhudi hizo ni sharti pawe na mikakati maalumu itakayohakikisha kwamba ajira ya watoto inazikwa katika kaburi la sahau.

Kulingana na ripoti ya shirika la kimataifa la wafanyakazi, kunao takriban watoto milioni mia moja na kumi na watano wanaofanya kazi katika mazingira hatari kote duniani. Inakadiriwa kuwa karibu watoto ishirini na wawili elfu, huaga dunia kila mwaka wakiwa kazini. Nao wale wanaonusurika huenda wakaathiriwa pakubwa kiafya ukubwani mwao.

Baadhi ya watoto hao wameajiriwa katika migodi machimbo ya mawe, mijengo, na hata mitoni wanakozoa kizingo. Maeneo haya yana hatari nyingi sana. Ikumbukwe pia wafanyikazi katika maeneo haya aghalabu hawana mivao maalumu kuwakinga dhidi ya kudhurika. Baadhi ya athari zinazotokana na mazingira mabovu ya kufanya kazi, ni pamoja na maumivu kwenye viungo, mikono, kiuno na hata mgongo. Aidha,

c \

282 wao hupatwa na matumbwitumb-kwenye miguu na mikono.

Mara kwa mara wengi huug.: maumivu ya kifua, kikohozi kisichois-: na kuugua ugonjwa wa pumu. Wengir* huenda wakaugua mapafu kutokana n: kupumua hewa chafu iliyojaa vumbi la pc t kazini. Vilevile wengine hupata maradhi kifua kikuu kutokana mazingira mabo.. na kukosa lishe bora.

Navyo vifaa vya utendeaji kazi huenc: vikadhuru neva na kuzorotesha msukurr: wa damu mwilini. Hali hii inawez; kusababisha ukosefu wa hisi mwilini. Wakati mwingine kufanya kazi kwenie jua kali huwa na madhara tumbitumb Miongoni mwa athari hizo ni uchunc. machoni, mwasho wa ngozi na upunguf. mkubwa wa maji mwilini.

Matumizi ya mara kwa mara u: dawa za kupunguza maumivu yana athcr kubwa sana. Mwanzo humfanya mtumic kuwa mraibu wa dawa hizo. Pili, huathir viungo mwilini hususan ini.

Suala la ajira sharti liangaziwe imc fa ima, kuimarisha maisha ya watu wake na hasa kuhakikisha kwamba watotc hawadhulumiwi kupitia ajira ya mapema.

## Maswali

1. Chagua jibu sahihi kutokana nc kifungu ulichokisoma

A. Watoto wengi wameajiriwa na shirika la kimataifa la wafanyakazi.
B. Kupunguza kiwango cha umaskini ni kati ya malengo ya milenia.
C. Takriban watoto ishirini na wawili elfu hunusurika kufa wakiwa kazini.
D. Ni muhimu kubuni njia maridhawa za kuimarisha ajira ya watoto.

2. Maana ya 'wanakozoa kizingo' kulingana na ufahamu ni ipi?

A. Wanakoondoa tope maalumu la kufinyanga vyungu.
B. Wanakosomba mchanga unaotumika katika ujenzi.
C. Wanakosambaza nyavu za kuvulia samaki.
D. Wanakookota mawe. yanayotumika katika ujenzi.

3. Ni jukumu la nani kuafikia malengo ya milenia?

A. Watoto wote duniani.
B. Wafanyakazi wote kwa jumla
C. Shirika la kimataifa la wafanyakazi.
D. Wanajamii wote.

4. Madhara yanayowapata watoto kazini si pamoja na

A. kuugua ugonjwa wa mapafu.
B. kuumwa na viungo vya mwili.
C. kuharibika kabisa kwa neva mwilini.
D. kupata uvimbe mikononi au miguuni.

5. Janga la ajira ya watoto litamalizwa na

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

A. kubuni malengo mapya ya milenia.
B. kuajiri watoto katika mazingira yasiyowadhuru.
C. kupunguza idadi ya watoto wanaoajiriwa katika mazingira mabovu.
D. kuboresha hali ya maisha ya wananchi wote.

6. Idadi ya watoto wanaofanya kazi katika mazingira duni ni ngapi?
A. 100,000,115 B. 110,000,015 C. 100,000,015 D. 115,000,000

7. Kwa mujibu wa taarifa ni kweli kusema kuwa
A. ajira ya mapema ina mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi.
B. dawa za kupunguza maumivu zinaweza kudhuru viungo vyote vya mwili.
C. uwezo wa kuona vizuri unaweza kupunguzwa kutokana na jua kali.
D. ni vyema kuajiri watoto bila kuwadhuru.

8. Maana ya neno 'inakadiriwa' kama lilivyotumiwa katika ufahamu ni
A. inakisiwa B. inafahamika C. inaenezwa D. inadhaniwa

9. Kwa mujibu wa kifungu, 'inazikwa katika kaburi la sahau', ni tamathali gani ya lugha imetumika?
A. Nahau B. Methali
C. Shada D. Istiara

10. Kulingana na ufahamu, kinachochangia hasa kudhurika kwa wafanyakazi kazini ni .
A. kupumua kwa chafu
B. ukosefu wa mivao maalumu.
C. kufanya kazi kwenye jua kali.
D. kupungukiwa na maji mwilini.

## Kifungu cha sita

**Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 1-10**

Baada ya kutoka Burma, Utubora alisimama katika afisi mbele ya tajiri wake kumwambia kuwa alitaka kuacha kazi. Kazi yake ilikuwa ukarani katika afisi kubwa ya biashara ya karafuu. Mshahara wa Utubora ulikuwa simulizi karibu Unguja nzima; ilisemwa kuwa uliwatia wivu watu wengi sana. Alianza kazi kwa mshahara wa shilingi mia kwa mwezi kabla ya kuenda Burma. Aliporudi Unguja alishika tena kazi yake kwa mshahara wa shilingi elfu kila mwezi. Hata katika afisi za serikali hapakuwa na karani aliyekuwa akipata mshahara kama huo.

Utubora alistahili sana ijara kubwa kama hiyo kwa sababu ya sifa alizokuwa nazo. Alikuwa mtu imara mbele ya telezi nyingi, kama vile hiana na mengine; mvumilivu mbele ya majaribu magumu kama rushwa; hodari mbele ya mashaka mazito, mfano wa kushika au dhima kubwa; mwaminifu kama mchana na msiri kama usiku. Kwa kushika majira alikuwa kama saa; na mahudhurio mema katika kazi hayakuwezekana kushindwa na

r \
283

2. Wakati vyura walipoanza kukoroma wadudu
A. wakaanza kuruka japo kwa utulivu.
B. nao pia wakaanza kupiga kelele.
C. walijitoma kidimbwini na kujificha na vyura.
D. walifululiza mwendo na kujificha nyasini.

3. Yule kondoo alijibanza miguuni pa Amtala wakati upi?
A. Alipopigwa mateke.
B. Popo walipopuruka kati kwenye matawi ya miti.
C. Vinyama vidogovidogo vilipazidi kuimba usiku huo.
D. Fisi alipotoa mwangwi wa vicheko.

A. Chura hukoroma, kondoo, akaghorora nao ndege .
A. hukorokocha
B. hukiriza
C. hutetea
D. hutarakanya

5. Kwa mujibu wa taarifa, kilichowasitisha fisi ni nini?
A. Mgororo mkali wa kondoo.
B. Kutimka mbio kwa kondoo akiwakabili.
C. Kusimama wima kwa kondoo.
D. Kutoa sauti ngeni kwa kondoo.

6. Ule mwanga wa manjano aliouona Amtala ulitoka kwa
A. mapepo ya usiku.
B. kimondo.
C. taa za wanavijiji walioishi mbali na pale alipokuwa Amtala.
D. wasafiri waliokuwa wamechelewa.

7. Neno 'mwangwi' kama Ulivyotumika kwenye taarifa Una maana gani?

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

A. Vicheko vya fisi.
B. Sauti ya kondoo iliyoashiria hatari.
C. Sauti ya kurejelea.
D. Sauti ya mikanyago ya fisi walimkaribia Amtala.

c \
286

8. Jambo lisilojitokeza katika taarifa I ni kuwa .
   A. Amtala alikuwa ameenda machungani na nduguye.
   B. kidimbwi hakikuwa mbali sane na baraste.
   C. wasafiri kadhaa walijipata barabarani usiku.
   D. Amtala alitawaliwa na hasira.
9. Kauli ipi ni kweli kulingana na kifung.
   A. Yule kondoo aliwaelekeza wanaume hadi alipokuwa Amtala.
   B. Sauti ya vyura na wadudu ilimwongoza kondoo hadi alikokuwa Amtala.
   C. Afua ya Amtala ilikuwa katika kupaza sauti.
   D. Fisi walimfuata yule kondoo na kumwacha Amtala.
10. Ni kwa nini yule kondoo alikuwa nc Amtala?
   A. Alimthamini sana Amtala.
   B. Hakupenda kuelekezwa nyumbani na nduguye Amtala.
   C. Alipotea njia mifugo ilipokuwa ikielekezwa nyumbani.
   D. Alihofia maisha yake na ya Amtala aliposikia sauti ya fisi.

## Kifungu cha nane

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu **maswali 1—10**

Ulimwengu una elimu ya kuishi na elimu ya kufa. Mtu kufa kitandani pake, katika nyumba yake ni rahisi kabisa. Si kifc cha heshima. Ni mwisho usio na maana katika maisha. Lakini wale wafao kwa ajili ya tendo bora kama vile kupigania uhuru wa taifa au ulimwengu, kusaidia watu wanaodhulumiwa na wenye dhiki wanaodhalilishwa, hufa kifo kitukufu.

Wafao katika tendo bora hawafi, kwa sababu majina na sifa zao hazisahauliki. Kifo cha mwili hakikomeshi maisha yao. Huishi katika kumbukumbu za mioyo

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

ja watu. Wao peke yao ndio wenye nafanikio katika maisha.

Wengine walao, wanywao na vachezao hawafanikiwi katika dunia. Yameshindwa. Lakini hawashindwi wafao <wa tendo bora.

Mtu hutupa maisha yake katika aitengeneza maslahi au siasa au dini. Huenda akashindwa kutimiza natengenezo yote katika wakati wa uhai »vake, lakini kazi aliyoianza huendeshwa na wengine kwa kupokezana kwa zamu <ama mwenge uliowashwa au vijiti katika nbio. Mtu huyo huwa mfano kwa wengine. Ni kigezo cha kuigwa. Kwa hivyo, hata akishindwa, hufanikiwa.

Kushindwa kwake ni mwanzo wa <ufanikiwa kwa wengine. Wafao vitani <wa sababu ya uhuru, hawafi. Ni mashujaa nafahari ya nchi katika kumbukumbu zetu. 3aadhi ya watu hutupa maisha yao katika elimu, uvumbuzi, uganga na matendo mengine ya thamani. Hawashindwi wala hawafi kwa sababu hutenda mambo bora.

Mtu afaye fofofo ni mtu afanyaye kazi ya manufaa yake mwenyewe na tumbo lake. Chambilecho Ustadh Guru, "Hao ndio watu wa ubinafsi, tumbokarai!"

## Maswali

1. Taarifa inatuambia kwamba katika ulimwengu
   A. watu wanajifunza elimu ya kufa na ya kuishi.
   B. mwanadamu anakabiliwa na kuishi na kufa.
   C. mtu hufa kitandani pake.
   D. ni rahisi kufa kifo cha heshima kitandani.
2. Mwandishi anasema, mtu kufa kitandani pake si kifo cha heshima kwa sababu
   A. atakuwa amekufa kibudu.
   B. ni kufa bila matendo bora ya kukumbukwa.
   C. amekufa kwa urahisi kabisa.
   D. hana elimu ya kuishi na kufa.
3. Wafao katika tendo bora hawafi, maana yake ni
   A. wanaishi daima dawamu, milele na milele.
   B. huenda kustarehe mahali pema peponi.
   C. hukumbukwa daima pamoja na matendo yao.
   D. mashujaa wasiodhurika maishani.

A. Taarifa inatudokeza kwamba walioshindwa ni watu gani?
   A. Wazembe wapenda anasa.
   B. Mashujaa wapigania uhuru.
   C. Wenye elimu ya kuishi na kufa.
   D. Wasiowania kula, kulewa na kucheza.

5. Mtu hutupa maisha yake ... Neno "hutupa" limetumika kwa maana gani katika taarifa hii?
   A. Anatupatia.
   B. Hurusha kwenda mbali.
   ■ C. Hutumia.
   D. Huharibu bure bilashi.
6. Mwenge na vijiti katika mbio vimetumiwa katika taarifa hii kurejelea
   A. kuishi na kufa.
   B. matendo mema na maovu.
   C. kutenda matendo mema na kusahaulika.
   D. kuanza matendo mema na kuwaachia wengine wakiyaendeleza.
7. Katika taarifa hii, maneno akishindwa, hufanikiwa yametumiwa kama
   A. maneno ya visawe.
   B. maneno ya vitawe.
   C. maneno ya vinyume.
8. Katika aya ya mwisho, msemaji anatuambia
   A. mtu anaweza kushindwa akafanikiwa.
   B. kushindwa kwa mtu mmoja kwaweza kuleta mafanikio kwa watu wengine.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

C. watu huwa hawafi vitani.
D. mashujaa wa uhuru hawafi.

9. Mtu anayejipenda, mwenye ubinafsi, matendo yake yamemithilishwa na
A. Ustadh Guru akiwaita tumbokarai.
B. mtu aliyekufa fofofo.
C. aliyefanya kazi ya manufaa.
D. mzalendo kindakindaki.

10. Kichwa kinachofaa zaidi kwa taarifa hii ni:
A. Kuishi na kufa.
C. Maisha bora.
B. Kufa fofofo.
D. Matendo mema.

## Kifungu cha tisa

Soma kifungu kifuatacho kwa makini kisha **ujibu maswali 1—10**

Kwa lugha ya Kiingereza pametokea taifa la Waingereza wa nchi ya Uingereza. Waingereza, Wawalase, Waranda na Wasikochi walikuwa watu wa mataifa mbalimbali zamani. Lakini wameungana taifa moja sasa. Nao wakakubali kwamba Kiingereza kuwa lugha ya Uingereza. Aidha kuna mataifa mengine mengi tu ambayo yameungana kuwa taifa moja lenye lugha moja na watu wamoja walio na lugha moja kama vile Ujerumani na Kijerumani, Ujapani na Kijapani, Uchina na Kichina, Urusi na Kirusi, Ureno na Kireno.

Namna moja ya maarifa ya siasa na utawalahaviunganishi watu pamoja. Lugha ndicho chombo kitendacho kazi muhimu katika kuleta mapatano, uelewano na malezi mema ya kweli ulimwenguni.

Bahati njema, Afrika Mashariki tuna Kiswahili kiwezacho kuwaunganisha vema watu wetu kuwa taifa moja. Ni bahati mbaya iliyoje kwa baadhi ya watu kufikiri kukivunja Kiswahili kisitumike? Hasara kubwa iliyoje kwa warithi wa ukoloni na vizazi vya leo kukosa kuungana! Hawajui kuwa umoja ni nguvu utengano ni udhaifu?

( ^
288

Lugha ya Kiswahili ina nguvu mkuweza kushindana na upinzani wov,**rzr** ulimwenguni na kuushinda. Inaw;: kuleta maendeleo makubwa zaidi lichc ya mwungano na uelewano katika Afrika Mashariki na bara zima la Afrika.

Kiswahili ni lugha maarufu na muhirr. sana ulimwenguni. Inatumika katik: nyanja zote za elimu na teknolojia karr: vile katika mitandao, tarakilishi, tovuti r; mawasiliano ya kilimwengu. Inatangazv.; katika idhaa za mataifa makubwa mitr ya Ujerumani, Uingereza, Uchinc Marekani, Urusi, Ujapani na kwingineko.

Kiswahili hutumika katika uandisr wa vitabu, majarida, nyaraka na magaze: ya kila siku katika mataifa mengi. Karr: huo si ubora na umaarufu, basi udufu ukc wapi?

Ama kwa hakika, nchi zetu za Afrikc Mashariki, Kenya, Uganda na Tanzanic tuna udhuru gani wa kuipuuza lugha yc Kiswahili hadi kuinyima nafasi ya kukuzc uzalendo wetu na kuimarisha umoja tulic nao?

Tuna haki ya kuona fahari kuitumic lugha ya Kiswahili kwa hali na ma Tutatambualini kuwa Kiswahili ni miongor mwa lugha kuu za ulimwengu? Wangap wajuao hivyo kama si Mheshimiwa Rais wc Msumbiji, Joakim Chisano na Mheshimiwc Rais wa Tanzania, Jakaya Kikwete, ambac wamewahi kuhutubia vikao vya mikutanc ya Umoja na Nchi Huru za Afrika kwc lugha ya Kiswahili? Vipi mimi na wewe Tunajivunia Kiswahili?

Naam, kama Kiingereza ni kwc Waingereza wa nchi ya Uingereza, sisi na Kiswahili chetu hatuwezi kuwa na Kiswahi. kwa Waswahili wa Uswahili badala ya kujigawa katika vijitaifa na vijikabila hi\ tulivyo navyo? Tunachelea nini? Tunangojc nini? Mpaka lini? Ipo siku.

Nasaha za: Guru Ustadh Wallah Bin Wallah katika hafla, Arusha 2006.

## Maswali

1. Kauli ipi ni sahihi kulingana na aya ya kwanza ya taarifa hii?
A. Mataifa mbalimbali yaliungana kuunda taifa kuu la Uingereza.
B. Waingereza waliungana na mataifa mengine kuunda nchi ya Uingereza.
C. Lugha ya Kiingereza iliunganisha taifa la Uingereza na mataifa mengine kuwa taifa.moja.
D. Lugha ya Uingereza iliwaunganisha Waingereza wakawa taifa moja.

2. Taarifa haisemi kwamba
A. hakuna mataifa mengine yaliyounganishwa na lugha yakawa moja ulimwenguni.
B. Ujerumani, Ujapani, Uchina, Urusi na Ureno ni mifano ya Uingereza.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

C. Uingereza ni muungano wa mataifa zaidi ya moja.
D. lugha ya Kiingereza ilitumiwa kuyalazimisha mataifa mengine kuungana.

3. Mwandishi anasema kwamba
   A. maarifa ya siasa na utawala ni sehemu tu ya muungano wa watu pamoja.
   B. watu wanaweza kuungana vizuri wakiwa na maarifa ya siasa na utawala wa namna moja.
   C. muungano kamili wa mataifa na watu wake huweza kuletwa tu wakiwa na lugha moja.
   D. kila mtu ulimwenguni hupata malezi mema ya kweli akitumia lugha yake.

4. Katika Afrika Mashariki
   A. tuna bahati ya kuwa na lugha ya Kiswahili inayoweza kutuunganisha.
   B. Kiswahili kimepiga hatua kubwa na kuleta muungano kamili katika nchi zetu.
   C. tunapenda lugha ya Kiswahili lakini haiwezi kutuunganisha.
   D. Kiswahili hakitumiki vyema na watu wetu.

5. Watu wanaokitaka Kiswahili kisitumike kikamilifu ni
   A. walio na kasumba za kikoloni.
   B. wanaoogopa kusema Kiswahili.
   C. watoto au vizazi vya wakoloni.
   D. wanaotaka kurithi ukoloni.

6. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu ni methali iliyotumika katika taarifa kubainisha kwamba
   A. watu wakiungana watakuwa na nguvu.
   B. watu wa Afrika Mashariki wakitumia Kiswahili wataimarisha umoja wao wa kweli.
   C. tuna udhaifu mwingi kuliko umoja.
   D. hatuna nguvu bila umoja.

7. Lugha ya Kiswahili ina nguvu za kuweza kushindana na upinzani gani?
   A. Wa mataifa ya nchi.
   B. Wa wananchi wenye fikra za kikoloni.
   C. Wa kutumiwa na mataifa ya nje.
   D. Kutoka kwa maadui wa nje ya mataifa yetu na waliomo ndani ya nchi zetu.

8. Umaarufu na umuhimu wa Kiswahili vimedhihirika vipi?
   A. Kiswahili hutumika ng'ambo.
   B. Kiswahili hutumika katika mawanda yote ya elimu pamoja na mataifa ya ulimwengu.
   C. Rais Jakaya Kikwete na Joakim Chisano walikitumia katika mikutano yao.
   D. Afrika Mashariki tuna udhuru wa kukipuuza.

9. Mwandishi anatubainishia kwamba
   A. ipo siku Kiswahili cha Waswahili kitaunda taifa la Uswahili.
   B. Kiswahili hakiwezi kuleta umoja wa kweli ulimwenguni.
   C. ni muhimu kujigawa katika vijitaifa na vijikabila tulivyo hivi sasa.
   D. tumngoje mtu atuletee Kiswahili kituunganishe.

10. Anwani inayofaa zaidi kuelezea taarifa hii ni:
   A. Kiswahili chetu.
   B. Lugha ya Taifa.
   C. Matumizi ya Kiswahili.
   D. Ipo siku.

## Kifungu cha kumi

Soma kwa **makini taarifa hii kisha ujibu maswali 1-10**

Siku ilikuchwa vibaya kwa mvua, ngurumo na makeke ya umeme. Kwa hali hii, kila mahluki alilazimika kuenda kulala awali ya saa ya kawaida.

Mmuliko mmoja ulipenya nyumbani mwangu, mkawa mweupe kama kwamba mlikuwa na taa ya umeme. Dakika ile ile nilisikia mnazi ulioko uani ukianguka, na mbele barazani, nilisikia kitu kikichugachuga na kuchacharika. Nilituhumu kwamba kitu hicho kilikuwa kikibari mvua. Dhana zangu ziliniambia kuwa ni nyamaume mawindoni. Basi nikaupinda mgogole wangu kutoka unyayoni hadi utosini. Mara tu nikalala fofofo.

Asubuhi yake kulikuwa shwari na kutulivu. Nalo jua lilionekana kuwa kali licha ya kwamba ilikuwa saa kumi na mbili na nusu tu nilipoamka.

Basi nilikwenda kuufungua mlango huku moyo ukinisisimka na kunidunda dududu! Kule kuufungua tu, nikaona nyama kubwa

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

limekingama mlangoni. Pale pale, niliufunga mlango ndi kwa hofu na kuduwaa, nikisikiliza moyo ukinidunda. Nilidhani ni simba kama nilivyokisikia jana usiku. Halafu nikafafanua jinsi nilivyomwona tena, nikakumbuka kuwa nilimwona akiwa na hatamu na saruji. Niling'amua kwamba hakuwa simba.

Naam, nikaufungua mlango te Mnyama yule alinilaki kwa huzuni simanzi huku akiyakaza macho yatc* katika maiti aliyekasimiwa na kitu fulc-na aliyelala pale uani pangu.

Kwa kuwa nyumba yangu iliku karibu na barabara, nilifahamu kwam msafiri yule alikuwa akija kwangu kub mvua na kuepa dhoruba ile ya jana usi ndipo alipopatikana na mkasa ule.

Ama kweli, yake ilikuwa bah mbaya, kwani mbwa hafi maji aona~ ufuko. Maskini Kisigino, sikuwa na [c kufanya kwa muda wa nusu saa nzimc kwa butwaa lililonipiga!

## Maswali

1. Kwa nini watu walienda kulala mapema?
   A. Waliogopa kuvamiwa na majangili.
   B. Kulikuwa na vita nje.
   C. Waliogopa fujo na vurumai za hali ya anga zilizotokana na vishindo vya mvua.
   D. Walikuwa wakiwaogopa mahuluki.

2. Mvua, ngurumo na makeke ya umeme yalitokea wakati gani?
   A. Wakati wa usiku mchanga.
   B. Wakati wa alfajiri.
   C. Wakati wa asubuhi.
   D. Wakati wa mchana.

3. Mmuliko uliopenya nyumbani mwa msemaji ulikuwa wa
   A. askari waliokuwa kwenye doria.
   B. mweso wa umeme.
   C. kurunzi za majambazi.
   D. taa ya umeme.

4. Msimulizi alisikia mnazi ukianguka
   A. sambamba na alipouona mmweko.
   B. alipotuhumu kitu kikichugachuga.
   C. alipodhani kuna nyamaume mawindoni.
   D. alipoupinda mgogole kutoka unyayoni hadi utosini.

5. Mnyama aliyekuwa barazani pa msemaji alikuwa
   A. simba. B. nyamaume.
   C. farasi. D. maiti.

6. Msemaji alijifunika gubigubi kwa mgogole wake akalala fofofo kwa sababu
   A. aliliona nyama limekingama mlangoni.
   B. alimwogopa nyamaume.
   C. alikuwa akiwaepa wanaobari mvua.
   D. alishikwa na bumbuazi.

I Nini maana ya "kubari mvua"?
   A. Ni kujikinga ili kuepuka mvua isikunyeshee.
   B. Ni kuogopa mvua.
   C. Kuingia ndani ya mvua.
   D. Kurovya rovurovu kutokana na mvua.

8. Maiti aliyeonekana pale uani alikuwa nani na aliuawa na nini?
   A. Mwizi au jambazi aliyeuawa na nyamaume.
   B. Maskini Kisigino aliyeuawa na mvua.
   C. Saisi mpitanjia aliyeuawa na radi au mnazi.
   D. Mbwa aliyekasimiwa na mnazi.

9. "Mbwa hafi maji aonapo ufuko" ni methali iliyotumika katika taarifa hii kurejelea
   A. bidii za mbwa za kujiokoa.
   B. harakati za msimulizi kujibari mvua.
   C. msimumulizi alishikwa na butwaa alipomwona maiti uani pake.
   D. juhudi za marehemu yule kujiokoa licha ya mvua na makeke ya radi.

10. Kichwa mwafaka zaidi kwa habari hii ni:
   A. Mbwa hafi maji.
   B. Mvua ya tufani.
   C. Usiku wa kutisha.
   D. Maiti mlangoni.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

---------

* s
291

SEHEMU

5 Kuandika

## Hati au mwandiko

Hati ni mwandiko wa mkono kwa kutumia kalamu ama ni kwenye karatasi ai chokaa kwenye karatasi au chokaa kwenye ubao. Kuna hati za aina mbalimbali. Zote zinategemea mazingatio na mazoea ya mwandikaji mwenyewe. Wengine wanajitahid kuandika hati nzuri, bora na nadhifu sana ambapo wengine hawajali wala hawazingati ubora wa hati zao. Hata hivyo, ni muhimu kuandika vizuri kwa umakinifu ili maandish yako yawe yakisomeka bila vikwazo, shida wala utata wowote. Kumbuka, hati nadhifu ni kivutio kikuu kwa yeyote aisomaye insha yako. Je hati nadhifu au nzuri ni ipi? Nayc hati duni au mbovu ni ipi?

### Hati nadhifu na hati duni

| | Hati bora au nadhifu | Hati mbovu au duni |
|---|---|---|
| 1. | Yenye mpangilio mzuri wa herufi zilizochongwa na huandikwa vyema. | Herufi hazikupangwa vizuri, pengine zimechanganywa kubwa na ndogo. |
| 2. | Iliyoakifishwa vizuri kwa usahihi. | Isiyoakifishwa vizuri. |
| 3. | Iliyoandikwa kwa kalamu nzuri, siyo inayokwaruzakwaruza au inayofifia. | Isiyoandikwa vizuri kwa kalamu inayokwaruzakwaruza na maandishi hafifu yasiyoonekana vizuri. |
| k. | Inayosomeka vizuri, kwa urahisi bila matatizo wala kudodosadodosa. | Isiyosomeka vizuri wala kwa urahisi. |
| 5. | Inayokidhi haja na kiwango kinachohitajika cha ubora na urefu. | Isiyokidhi haja wala kiwango kinachohitajika cha ubora na urefu. |

## Imla

Imla ni hali ya mwalimu au mtu mwingine yeyote kutamka neno au maneno kutoka kichwani ama kitabuni ili kwamba msikilizaji (mwanafunzi) ayanukuu kwa usahihi.

### Madhumuni ya imla ni:

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

(i) Kupima uzingatifu, usikivu na umakini wa msikilizaji (mwanafunzi) kwa msemaji (mwalimu).
(ii) Kumzoesha mwanafunzi kuandika ama kuendeleza maneno kwa usahihi jinsi yanavyotamkwa na yanavyostahili kuandikwa.
(iii) Kumwezesha mwanafunzi kuakifisha kwa usahihi sentensi au aya kwa kuzingatia matumizi ya herufi kubwa na ndogo, alama za vituo, vikomo, viulizio, vishangao, vinukulu na kadhalika.
(iv) Kumwezesha na kumzoesha mwanafunzi kuyatambua na kuyachanganua aina za maneno katika kuyaendeleza, kuyatamka na tahajia.



Kwa makundi jifunze kuandika maneno haya:

### (i) Imla ya msamiati

| | |
|---|---|
| Ghali | Hila |
| Nang'anika | Kushtaki |
| Maridhawa | Kusherehekea |
| Thawabu | Tuliwahi |
| kumwudhi | Kurahisisha |
| Thubutu | Mandhari |
| Ghafula | Kimbiza |
| Madhubuti | Mandari |
| Rithi | Singizia |
| Aling'amua | Mbuga |
| Ridhi | Sinzia |
| Vumba | Bunga |
| Faragha | Fumba |
| Kushtuka | Hali |

### (ii)Imla ya sentensi

(a) "Mwanangu, unafanya nini?" mama alimwuliza.
(b) Lo! Kumbe alikuwa jizi!
(c) Tulinunua nyanya, nyama, vitunguu na dania.
(d) Juma ni mtoto wa Bwana Haji.
(e) Kaanga kanga lakini usichome kanga yako.
(f) Ali hali ilhali hana hali.
(g) Aliyeitwa alilie haliye.
(h) Chombo kinanuka shombo.
(i) Ametaalamika katika taaluma hizo.
(j) Mtoto yule amekua haraka na hivi sasa amekuwa mtu mzima.

# Insha

Inshanimtungowamanenoyanayotiririsha mawazo juu ya kisa, tukio, hadithi, maelezo, hisia au dhana yoyote kwa kutumia lugha sanifu; sentensi zilizopangiliwa vizuri na kuakifishwa vyema kwa nyakati mwafaka.

### Madhumuni ya insha

(i) Kumwezesha mwanafunzi kujieleza kwa usahihi na kwa ufasaha.
(ii) Kumsaidia mwanafunzi kupanga na kutiririsha mawazo yake.
(iii) Kumwongoza mwanafunzi kuzitumia mbinu nafani zote za lugha alizojifunza kama vile misamiati, semi, methali, tanakali, takriri, methali, nahau n.k.
(iv) Kumpa mwanafunzi fursa ya kutumia alama za uakifisho, herufi kubwa na ndogo pamoja na kuendeleza maneno kwa usahihi.
(v) Ni kipimo cha kujua uwezo wa mwanafunzi wa jinsi anavyotumia akili, busara na mantiki katika kuwaza na kubuni mambo, visa na maadili hadi kuyaeleza na kueleweka kwa kutumia lugha fasaha.
(vi) Kukuza na kujenga lugha ya mwanafunzi ili awe mtaalamu wa lugha siku zijazo.
(vii) Kumwongezea mwanafunzi ziada ya kupita mtihani wake wa Kiswahili.

## Aina za insha

### (a) Mdokezo

Mwanafunzi anadokezewa juu ya jamboauwazofulanikishaakatakikana aandike insha kutokana na mdokezo huo. Mfano: "Umechaguliwa kuwa Kiranja wa shule yako. Eleza jinsi utakavyotekeleza wajibu huu."

### (b) Dondoo/Mjalizo

Insha ya dondoo ni ya kuendeleza habari ambayo tayari imeshaanzishwa. Mfano: "Nilipozinduka kutoka usingizini nilijikuta niko peke yangu katikati ya wanyama wa kutisha. Mara..." Au, "Punde baada ya staftahi..."

### (c) Taswira

Ni kuandika insha kutokana na picha moja au picha kadhaa ili kwamba hadithi ipatikane kutokana na picha hizo.

### (d) Kimalizio

Katika insha hii, mwanafunzi hupewa neno au maneno ya kumalizia insha yake. Sasa ni juu yake kubuni jinsi atakavyoanza ili hadithi nzima ioane na mwisho au kimalizio alichopewa.

Mfano: Andika insha inayoishia kwa "Hivyo ndivyo nilivyoponea chupu chupu." Au "Sote tukaamini kwamba, kweli kikulacho ki nguoni mwako."

**(e) Methali**

Mwanafunzi anaweza kupewa methali yoyote ili aandike insha juu yake. Ni sharti aelewe maana ya methali hiyo. Na ni sharti aanze aya ya kwanza kwa kufafanua maana na matumizi ya methali yenyewe ndipo aanze kusimulia kisa kinachoeleza ukweli wa methali aliyopewa.

**(f) Barua**

Barua ni za aina mbili. Barua rasmi na ya kirafiki. Tofauti zilizoko katika barua hizi mbili ni mpangilio wa anwani zao, mianzo na jinsi ya kumalizia. Barua ya kirafiki/ kidugu ina anwani moja tu juu - upande wa kulia - na huanza kwa salamu baada ya kuandika jina la mpendwa unayemwandikia. Na barua rasmi au ya kuomba kazi au kitu , ina anwani mbili. Moja iliyo juu kabisa ni ya mwandishi na chini kidogo kushoto ni ya anayeandikiwa. Kisha huanza kwa kuandika kichwa au mada ambayo ni kiini cha hoja au maombi.

**(g) Kubuni**

Mwanafunzi anaweza kuambiwa aandike insha yoyote ya kubuni kuhusu hadithi au tukio lolote alitakalo mwenyewe. Insha hii ndiyo rahisi, bora na tamu kuliko zote kwani mwanafunzi ana nafasi, uwezo na uhuru kuichezea anavyotaka.

**(h) Maelezo/Masimulizi/Wasifu**

HYzi n'\ msha zinazomtaka mwanafunzi atoe maelezo au sifa juu ya mtu fulani, mahali au kitu fulani. Mfano: "Eleza jinsi ulivyozitumia siku za likizo." Au "Eleza sifa za mwalimu wako wa Kiswahili" au "Andika insha juu ya shule yako."

(i) Hotuba

Insha hii ina mtego wake. Mteg: huo hutegemea mwanzo au ufungu: jinsi utakavyoianza ili msomaji ajue unawahutubia, unaielezea nini nc unavyomalizia.

Mfano: Wewe ni chifu wa kitongoj chako, toa hotuba kwa wananchi wake ukiwaelezea umuhimu wa kuchemshc maji ya kunywa.

Au: "Ndugu wapenzi, leo nachukuc fursa hii kuwaelezea faida na manufac ya kuwaelimisha watoto wenu... Endeleza hotuba hii."

Tanbihi: Katika kuandika insha ya hotuba, ama unaweza kutumia alama za vinukizi mwanzo na mwishoni mwa hotuba tu, au usiinukuu.

Si lazima. Kwani kila mmoja atakuwa ameshajua kuwa msemaji au hatibu anayehutubu ni fulani.

(j) Mazungumzo

Insha inaweza kuwa ya mazungumzo au ya mahojiano kati ya watu wawili ama zaidi. Insha hii huandikwa kwa njia ya tamthilia. Mfano:

Andika mazungumzo kati ya daktari na mgonjwa ukianza hivi: Daktari: Jina lako nani, unaishi wapi na umeugua tangu lini?

Mgonjwa: Jina langu ni Goigoi, ninaishi Kanyariri na nimeugua tangu juzi.

Daktari: Umewahi kuenda katika hospitali yoyote?

**(k) Mjadala**

Inahusu hoja au mada yanayohitaji maoni ya pande mbili katika kuunga mkono au kupinga ili kupata suluhisho mwafaka.

Mfano: Afya ni bora kuliko mali. Jadili.

Kumbukumbu

Insha ya aina hii inatoa vidondoo vya hoja mbalimbali zilizojadiliwa katika mkutano fulani uliofanywa. Huanza kwa kueleza ni lini mkutano ulipofanywa, wapi na kina nani waliohudhuria na wepi ambao hawakuhudhuria na udhuru wao. Kisha huandikwa kwa kupangilia kumbukumbu kutoka ya kwanza hadi ya mwisho. Pengine: Kumb. 1/3/06: Mkutano ulifunguliwa kwa sala kutoka kwa Siti Miswaleh.

## Yaliyomo katika insha

a) **Anwani**

Ni kichwa cha insha ambacho ndicho huzaa maelezo na kiini kizima cha insha.

(b) **Maudhui**

Ni kiini au lengo maalumu la insha. Mtahiniwa hawezi akaandika tu habari au insha ambayo hailengi maelekezo aliyopewa. Na ikitokea hivyo husemwa insha imepotoka. Na mtahiniwa hukosa tuzo za maudhui ambazo ni takribani humusi ya alama zote.

**(c) Aya**

Aya ni kifungu kizima chenye ujumbe kamili katika insha. Insha ni mfululizo wa aya kadhaa. Kwa hivyo insha sharti iwe imeundwa kutokana na wingi wa aya kama tano hivi na kuendelea.

**(d) Lugha**



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Insha hujengwa kwa fani zote za lugha. Kukosekana kwa msamiati wa kutosha, misemo na mapambo yote ya lugha kama vile nahau, tashbihi, tanakali, methali na takriri ni kama kuandika insha ghafi, au chapwa.

**(e) Sarufi**

Lugha ya insha ni lazima iwe sanifu sana. Mtunzi wa insha bora sharti awe ameipamba kwa sarufi bora kwa mazingatio ya kanuni zote za ngeli.

**(f) Maendelezo**

Kila neno linalotumiwa katika insha hutazamwa kuwa limeendelezwa vizuri - yaani limeandikwa kwa usahihi.

**(g) Uakifisho**

Ndani ya insha huchunguzwa sana utumiaji sahihi wa alama zote za lugha pamoja na mpangilio wa sentensi. Aidha herufi kubwa na ndogo hazina budi kutumiwa kwa usahihi.

**(h) Mwandiko**

Ni muhimu kutumia hati nadhifu katika insha kwani hati ndiyo inayomvuta au kumkirihi msomaji wa insha ya mtahiniwa.

## Mazingatio katika uandishi wa insha

1. Andika anwani au kichwa, tena kwa herufi kubwa kisha upigie kistari chini.
2. Tumia hati safi inayovutia na kusomeka bila shida yoyote.
3. Pangilia vizuri insha yako kuanzia utangulizi, maelezo ya kiwiliwili na tamati.

k.Tumia lughafasaha, inayochangamsha na kuvutia mwanzo hadi mwisho.

5. Usichanganye lugha. Usitumie lugha mseto, Kiingereza wala ya mama hata neno moja. Kumbuka unapoandika insha ya Kiswahili utumie Kiswahili pekee.
6. Tia kila hoja au wazo katika aya yake. Usichanganye hoja au kujaza hoja nyingi katika aya moja.
7. Usilazimishe au usipachikepachike misamiati, misemo na methali ambapo havitakikani.
8. Tumia sentensi fupifupi, tena zinazoeleweka.
9. Urefu wa insha yako lazima ulingane na kiwango cha maagizo. Usiandike insha fupi sana au ndefu sana kuliko kiasi ulichoambiwa.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

## Insha bora

Ubora wa insha hutokana na ubora wa mwandishi mwenyewe wa insha. Na mtu hawezi kuwa bora katika kuandika insha pasipo kuwa bora katika kujua kusanifu, kusarifu na kusharifu sarufi ya Kiswahili. Na usanifu wa sarufi hutegemea kwa kiasi kikubwa utalaamu wa kutawala Ngeli zote na vipengele vyake - vivumishi, viulizi, viashiria, viambishi na vimilikishi. Kwa hivyo insha bora ni:

> "\
296

- Yenye anwani iliyoandikwa vizuri kwa herufi kubwa.
- Yenye mwanzo wa kuvutia.
- Iliyoandikwa kwa hati nzuri na nadhifu.
- Iliyoakifishwa vizuri.
- Hiyo na maudhui kamili kulingana na kichwa.
- Iliyotiririka vizuri.
- Yenye mpangilio mwema wa aya.
- Hiyo na lugha fasaha iliyozingatia ngeli zote.
- Iliyoandikwa kwa Kiswahili sanifu bila mseto wowote.
- Yenye maneno yaliyoendelezwa yote vizuri na sahihi.
- Yenye mawazo mazito, mapevu, maadilifu na mantiki.
- Yenye sentensi fupifupi na fasaha.
- Iliyoandikwa kufikia kiwango maalumu kilichotajwa.
- Iliyokamilishwa na kumalizwa vizuri na haswa kumalizwa kwa msemo au methali kuwa ndiyo sentensi ya mwisho.

## Mbinu za kuepuka kuandika insha duni

### Ukitaka uepukane na uandishi wa insha duni

- Usizoee kuongea lugha duni, shaghalabaghala.
- Usichanganye lugha duni na fasaha.
- Usichanganye lugha katika mazungumzo yako.
- Soma sana ngeli zote uzielewe barabara.
- Usitumie neno ambalo hulijui au hur: hakika hutumika vipi.
- Usipachike neno, msemo au methc ovyo tu.
- Soma vitabu vya riwaya au hadir fupifupi kila mara.
- Kila unapojifunza neno jipya au mserr: mpya uliokuvutia, jaribu kuutumia katik: sentensi.
- Usiandike kwa papara. Andika vidokez vyako kwanza pembeni.
- Jizoeze kuandika insha mara kwc mara. Usipitishe wiki (juma) moja bile kuandika insha. Ni bora zaidi kuandikc insha mbili hata tatu kwa juma moja nc umpe mwalimu akusahihishie.
- Jenga motisha ya kujifunza japo kwc insha fupi fupi.
- Jifunze mara kwa mara matumizi ya semi na methali kadha wa kadha rahisi rahisi.
- Hakikisha kwamba umewahi kukutana au kuliona neno lolote unalotaka kulitumia ili ujue linavyoendelezwa.

## Mbinu za kuandika insha ya kuvutia

Uandishi wa insha bora ni fahari ya mwanafunzi aliye makini katika kujifunza na kujiendeleza katika lugha. Hutokana na kujitahidi na kujibidiisha katika kujiongezea ujuzi kila mara na kila wakati.

### Hivi ndivyo jinsi ya kuandika insha bora:

- Hakikisha kwamba umejifunza ngeli zote na kuzielewa kikamilifu pamoja na kuzitawala.
- Kuwa mwangalifu kila unapoandika insha zako ili usifanye makosa madogo madogo ya kipuuzi.
- Panga vidokezi vyako kwanza kabla hujaanza kuandika baada ya kusoma na kuelewa kichwa.
- Weka kila kidokezi kimoja katika aya moja.

Tumia sentensi fupi fupi katika kila aya.

- Funga kila aya kwa msemo au methali.
- Tumia fani za lugha ili kuifanya insha yako ichekeshe au ichangamshe.
- Lazima uelewe kila insha ina madhumuni gani na usiipotoshe.
- Endeleza kila neno kwa usahihi. Daima tumia kamusi unapojifunza lugha - hasa maana na matumizi ya maneno.
- Tumia kila msemo kila panapohitajika kwa mfano, unapotaja sifa za ukubwa wa kitu au mtu usikose kuufananisha na nini. Ama unapotaja rangi - labda wekundu wake, umithilishe na damu; weupe umithilishe na theluji; ufupi ni kama nyundo au mbilikimo; mwanguko majini ni chubwi n.k.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

- Uandishi wa insha bora huhitaji mazoezi ya mara nyingi na mazoezi ya kusomasoma maandishi na hadithi kadha wa kadha bila kusahau ngeli.

## Sampuli za insha bora

### (a) Insha ya kubuni

Swali: Eleza jinsi ulivyopambana na mwizi Jibu:
Kupambana na mwizi. Vidokezi

| | | |
|---|---|---|
| Wazazi safarini. | 2. Kulala mapema. | 3. Usingizini. |
| Kishindo. | 5. Kuzinduka. | 6. Mapambano. |
| Kamsa. | 8. Polisi. | 9. Wazazi kurejea. |

USHIKWAPO SHIKAMANA

ngawa upweke ni uvundo, lakini mimi nililazimika kubaki peke yangu nyumbani. Wakati huu -dipo nilipong'amua kwamba heri jirani kuliko ndugu wa mbali. Kwani nilitamani angalau jirani mmoja aje kwetu anisaidie kukaa lakini wapi. Tamaa yangu ilikuwa bure bilashi. Nayo iliambulia zatupu. Wazazi walikuwa wameenda safarini na kuniacha peke yangu nyumbani. Nami ilinibidi libakie vivyo hivyo, kwani pasipo budi hubidi.

Niliandaa kijio changu mapema mapema. Mnamo saa kumi na mbili unusu jioni, nilikuwa mezani. Nilikula kwa wasiwasi kama mwasi. Nilikuwa na woga kama kunguru. Sikujali sana. NHikumbuka kwamba kwa mwoga ndiko huenda kicheko.

Baada ya maakuli hayo nilijibwaga kitandani nikiusubiri usiku ukomae. Ah! Liwalo na tiwe. Baada ya mapambano makali kichwani mwangu kuhusu jinsi ambavyo ningethubutu kulala katika bahari hii ya jumba peke yangu, hatimaye nilipata usingizi. Si wa pono. Wa mang'amung'amu. Yaani sikulala fofofo. Nililala kama sungura. Nilivumilia nikijua dhahiri shahiri kuwa mvumilivu hula mbivu.

Kishindo kikali ndicho kilichonigutusha kutoka usingizini. Moyo ulinienda mbio. Sikujua ni nini. Nilihema haraka haraka kama mbwa aliyenusurika kumezwa na chatu. Nikatega sikio ndi. Mara nikaanza kupata hisi na fahamu zikaninyemelea taratibu kama jongoo. Ama kweli, nyumba ya udongo haistahimili vishindo.

Nilizinduka na kukaa kitako kitandani. Nikakodoa macho. Sikuona chochote. Mote mle chumbani mlikuwa na giza totoro. Kwa hivyo kuona kitu kulikuwa sawa na kumtafuta paka mweusi gizani. Kimya. Kimya kingi kina mshindo. Kumbe mlikuwa na pwagu mumu humu chumbani. Alijibanza pembeni akanipima na kunipa muda. Naam, nilimwona. Sasa nikajua r. pwagu atapata pwaguzi.

Niliupeleka mkono wangu nyatunyatu kwenye mchango nikatoa sime. Kufumba -: kufumbua nilimwahi mkwapuzi yule. Nikamtia dharuba ya utosini. Alipiga ukemi wa kutisha -<: kunirushia pandikizi la rungu likatua begani. Nilihamaki na kushikwa na kiruu mithili ya sirr:*: aliyejeruhiwa. Nikamvurumishia pigo jingine ambalo niliamini lingalimsafirisha jongomeo b : nauli lakini wapi. Hakukata kamba lakini alilala sakafuni mahututi akichungulia kaburi.

Niliporidhika kwamba nimemweza kiasi cha kwamba asingeweza kunidhuru ten nilipiga kamsa. Maadam sikuwa na hakika kama alikuwa peke yake au lilikuwa genge zirri nilijaribu bahati yangu kujihami kwa mayowe hayo. Hala hala mtu na jirani. Jirani waliwas'di -: kushuhudia ujasiri wangu. Walijua sikutumia nguvu bali akili kwani akili ni mail Na mapambc: huhitaji akili si mabavu.

Baada ya mashauriano machache, tuliamua tuwapigie simu polisi. Haukupita mucz kikosi kizima kiliwasili kwa vishindo na mori. Jambazi lile lilipigwa upya. Lilipigwa kipopo m kulia kama mbuzi lakini kilio si dawa na dua ya kuku haimpati mwewe.

Usiku huo ulikuwa wa hekaheka na mazingaombwe hivyo. Lakini kulikucha. Mchar: takriban saa sita adhuhuri, wazazi waliwasili wakiwa tayari wana habari. Walinipongeza m kunituza tunu tele na tamasha. Ama kweli, mcheza kwao hutuzwa au la hushangiliwa.

### (b) Insha ya barua

### (i) Barua za kirafiki/kidugu

Barua ni maandishi yenye ujumbe yanayopelekwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Barua za aina hii huandikiwa ndugu, jamaa, wazazi au marafiki.

f \



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

## Madhumuni ya barua za kidugu

- Kujuliana hali.
- Kushukuru.
- Kushauri.
- Kuonya.
- Kufahamisha.
- Kualika.
- Kuomba msamaha.
- Kutoa habari za tanzia.
- Kutoa pole.

## Muundo wa barua ya kirafiki

### Anwani

- Barua ya kirafiki huwa na anwani moja.
- Anwani huandikwa upande wa juu kulia katika karatasi.
- Huwa na jina la mtaa au kitongoji, jina la shule na sanduku la posta. Tunawashauri wanafunzi kuandika anwani kwa herufi kubwa.

### Mifano

SHULE YA MSINGIYA KARIOMBANGI,
SANDUKU LA POSTA 156-00050 NAIROBI.

MTAA WA TU FAH A,
SANDUKU LA POSTA 19009 - 00200
PARACHICHI.

### Tarehe

- Tarehe huonyesha wakati ilipoandikwa barua.
- Huandikwa chini ya anwani.
- Huweza kuandikwa kwa namna mbalimbali.

### Mifano

3-3-2015/ 15.8.2016/ 23 Januari,2017 n.k.

### Utangulizi

- Sehemu hii huandikwa baada ya anwani.
  - Huwa upande wa kushoto kuanzia kwenye pambizo.
  Huonyesha jina la anayeandikiwa.

### Mfano

Mama mpenzi Mwanaisha, Kwa baba mpendwa, Kwa msena Zawadi, Dada mpendwa Hilda,

### Mwili/sehemu kuu

- Maudhui ya barua huandikwa katika sehemu hii kwa mtindo wa aya.
- Aya ya kwanza huwa na salamu na kujuliana hali.
- Sehemu inayofuata huwa ni madhumuni ya barua yenyewe.
- Hoja huandikwa moja baada ya nyingine. Muhimu zaidi ni kuhakikisha kuwa, hoja imekuzwa vyema. Jambo jingine ni kuhakikisha hakuna kujirudia.

### Hitimisho

Huwa ni ujumbe wa mwisho katika mwili wa barua ambao huandikwa katika aya ya mwisho.

### Maagano

Maagano huwa ndiyo sehemu ya mwisho katika barua.
9
Sehemu hii huonyesha jina la mwandishi na uhusiano wake na anayemwandikia. Uhusiano huo huonyeshwa kabla ya kuandika jina.

Barua ya kirafiki haitiwi sahihi.

### Mifano

1. Ndimi msena wako wa kufa kuzikana, Sadiki Ukipenda.
2. Ni mimi mzazi wako mpendwa, Naisura Kauchape.

### Mifano

### Kielelezo cha kwanza

Shule ya msingi ya Asalichungu,
Sanduku la Posta 1810-00200,
Heroe.

2 Agosti, 2016.

Mwanangu mpendwa Vumilia,

Pokea salamu tumbitumbi mithili ya changarawe katika jangwa. Je, u hali gani pamoja na wanafunzi wenzako? Nina hakika ya mauti kuwa, rai zenu ni aula. Mimi ni mzima kama ngarange za mivule na imara kama chuma cha pua. Namshukuru Dayani kwa kunipa zihi njema. Ninayo nyemi fokofoko kwa kuwa na mwanangu mwaminifu kama mchana na msiri kama mvaa buibui. Ninakupeza sana. Bila wewe katika likizo hii najiona kama aliyeachwa jangwani peke yake nao upweke ni uvundo. Hata hivyo afadhali kufariki kuliko kufa.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Azma ya kukuandikia waraka huu, ni kukupa nasaha kutokana na barua uliyoniandikia. Safari ya maisha ina milima na mabonde. Hi kufanikiwa katika mustakabali wako, huna budi kutia idili za mchwa wanaojenga kingulima kwa mate. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Tangu ulipojiunga na shule hii mpya, mwaka mmoja uliopita, nimeona umeimarika sana katika elimu. Ulikuwa na matatizo chungu nzima katika kila somo. Alama mia mbili ulikuwa hufikishi. Sasa ni afadhali maadamu unafikisha alama mia tatu kila wakati. Pokea mkono wa tahania.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Wahenga walipoamba, mficha uchi hazai. Nawe umenieleza mambo yote kuanziaukc-hadi utando. Awali ya yote umesema chakula si kizuri. Ndivyo wasemavyo wasena wako.l/s/'w* benderainayofuataupepo.Borachakula kinapatikana na hakina madhara yoyote, sioni tatizc hapo. Malalamiko ya chakula yalianza tangu, nyakati za alfu lela ulela.

Katika upande wa teknolojia, unasema mpewe nafasi ya kutumia rununu mtakavyo. HHi mimi naona halina natija yoyote. Labda wakati wa masomo husika. Vijana wengi wameanza kuwa na nyendo benibeni kutokana na matumizi ya mitandao. Sisemi rununu ni mbaya ila ni sharti tujue kuteua kati ya nyamafu na nyamachinje.

Jambo ambalo limenitia kimuyemuye zaidi ni hili mnalosema mkubaliwe kutangamana na wenzenu wa kiume. Pia mnasema kuwa mnaadhibiwa mkipatikana mmesuhubiana. Ni sharti mjue kila kitu kina wakati wake. Aidha kuna maradhi ya zinaa na UKIMWI. Usisahau wasichana wengi wameacha masomo kwa sababu ya kupata himila.

Uhuru wa kwenda mahali mnapotaka ni hatari. Ndiyo maana umesikia vijana wengi wamenaswa na mitego ya ulanguzi wa mihadarati. Huna budi kutahadhari kabla ya hatari.

Sina zaidi mwanangu. Endelea kutia bidii katika mambo yote yenye manufaa. Kumbuka ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

Inshallah tutaonana wakati wa likizo. Wahenga waliamba, waraka ni nusu ya kuonana.

Ndimi baba yako mpenzi,

Adabu Ufanisi.

## KCPE SWALI LA BARUA YAKIRAFIKI

| INSHAZAKCPEKISWAHILI1995-2011 | | |
|---|---|---|
| Mwaka | Aina ya Insha | Insha yenyewe |
| 1995 | Barua ya kirafiki | Mwandikie barua rafiki yako anayeishi mbali ukimweleza juu ya mambo yaliyotokea tangu mwaka jana pale unapoishi. |
| 2007 | Barua ya kirafiki | Rafiki yako amehamishwa na kujiunga na shule nyingine. Mwandikie barua ukimwelezea maendeleo yako tangu mlipoachana. |
| 2011 | Barua ya kirafiki | Mwandikie rafiki yako barua huku ukimshauri namna ya kujiandaa katika mtihani wa KCPE. |

## Mazoezi

1. Mwandikie baba yako au mama yako au jamaa mwlngine barua ukimweleza hali ilivyo katika shule yako na jinsi unavyojiandaa kwa mtihani wa kitaifa wa darasa la nane mwaka huu.
2. Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza kuhusu likizo ya Disemba baada ya kufanya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane.
3. Mwandikie binamu yako aishiye mbali na wewe barua ukimweleza juu ya tamasha ya muziki uliyohudhuria.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

-. Mwandikie rafiki yako barua ukimweleza juu ya maisha ya shule mpaka sasa.

5. Mwandikie mzazi wako barua ukimwomba akufanyie jambo fulani. Tumia lugha ya kushawishi ili akubali kukutekelezea ombi lako.

6. Rafiki yako mmoja mnayesoma naye katika darasa la nane amekosa kufika shuleni kwa muda wa muhula mmoja kwa kuwa alikuwa mgonjwa. Hivi sasa amepata nafuu ingawa hajafika shuleni. Mwandikie barua ya kumfariji.

Mfano wa barua ya kirafiki

KIWANDA CHA KOROSHO, S.L.P
170, KAZAMOYO. 6 - 12 - 2006.

Dada mpenzi Stella,

Salaam sana. Natumaini u hali njema buheri wa afya. Bila shaka unaendelea vyema na masomo jako huko shuleni Nguvumali. Mimi huku sina neno, hofu na mashaka nijuu yako tu. Ni mzima kama kigongo. Ninajitahidi kwa hali na mali kupambana na maisha katika harakati zangu za jjenzi wa taifa.

Baada ya salaam, ningependa kuchukua fursa na satua hii kukufahamisha na kukuelewesha kwamba ninaendelea vizuri na kazi zangu katika shirika hili la kubangua korosho mjini Kazamoyo.

langu niajiriwe hapa mwaka jana, Mungu amenijalia siha njema. Sijalala wala kuugua nikakosa kuenda kazini. Hiyo ni baraka kubwa sana dada yangu. Kwani afya ni bora kuliko mali. Licha ya hivyo fursa na mwanya wa kupata ajira ni finyu mno kiasi cha kwamba, endapo mja ni wa kuuguaugua huenda ukapigwa kalamu wakati wowote. Kumbuka, siku hizi ajira zimeadimika kama wali wa daku. Ama kusaka ajira ni sawa na kumtafuta paka mweusi tititi katika giza totoro. Naam asiye na bahati habahatishi.

Juzi nilipata muda na wasaa wa kuwasiliana na wazazi. Nina furaha kukujulisha kwamba, nilitumia mshahara wangu wa kwanza kuwanunulia rununu. Baba ana yake naye mama anayo. Kama si maendeleo, ni nini basi? Walifurahi wakanipongeza na kushukuru wakisema, ama kweli, kuzaa ni sudi.

Katika kuwasiliana kwetu, wazazi walinifahamisha kwamba hali zao shwari na mufti kabisa. Wadogo wetu wote Sadiki na Safia wako salama salimini. Wana bidii za mchwa katika masomo yao. Sadiki alishikilia nafasi ya pili katika matokeo ya mtihani waliofanya mwishoni mwa muhula uliopita ilhali Safia akawa nambari moja katika darasa lake. Kwa mintarafu hiyo, jana niliwatumia zawadi na tuzo tunu tunu pamoja na pongezi chekwachekwa. Waama, chanda chema huvishwa pete na mcheza kwao hutuzwa au la hushangiliwa.

Vipi upande wako? Masomo yanakuendea vipi? Ninavyokujua na kukuelewa, wewe ni mchapa kazi. Wema wako na uadilifu wako ni ngao kama si silaha katika kukusaidia masomoni. Bila shaka bado ungali ukiongoza darasani. Unajua dhahiri shahiri kwamba siri ya mafanikio ya mwanafunzi shuleni ni adabu, nidhamu na intidhamu za hali ya juu. Bahati iliyoje dada yangu kwamba wewe u mtambuzi na mwelewa wa hayo. Mwenyezi Mungu atakuruzuku riziki zake. Kumbuka, Mungu kasema, mkiniomba nitawapa. Na atafutaye hachoki, akichoka keshapata.

I Sina zaidi. Uwasalimie rafiki zako wote. Umwambie mwalimu wako wa Kiswahili kwamba sijasahau ahadi yetu ya kumtumia kitabu cha Taswira ya mtihani. Nitatimiza. Kwani ahadi ni den). Na dawa ya den) ni kulipa.

Ndimi,
Kaka yako mpendwa,
Avensis Tieksi.

## (ii) Barua rasmi

Barua hii pia huitwa barua ya ofisi au barua ya kikazi. Aghalabu ni barua inayoandikwa maalumu kwa ajili ya ombi fulani Umbo la barua hii huwa na:

- Anwani mbili; moja ya mwandishi na ya pili ni ya anayeandikiwa.
- Tarehe.
- Mada, mintarafu au yahusuyo.
- Maelezo na maombi yenyewe.
- Tamati na jina la mwandishi pamoja na sahihi.

Umbo **la barua rasmi**

- Anwani ya mwombaji au mwandishi na tarehe.
- An ya huandikwa kwa herufi kubwa. Na unaweza kuanza kwa namna tofauti hivi.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

1. MINT: KUOMBA KAZI AU
2. KUH: NAFASI KATIKA JESHI
3. KUMB: KUJIUNGA NA CHUO CHAKO

0 Ni maelezo. Mwombaji hutoa maelezo na maombi yake kadiri ya kuridhisha. Na kuzingatia urefu wa insha kulingana na maagizo.

- Nasaha. Haya ni maneno ya mwisho ambayo hutolewa na mwombaji kwa sentensi moja tu.
- Wasalaam tamati, jina na sahihi ya mwandishi. Huo ndio mwisho (Wako, Mwaminifuau Wako Mtiifu).

Mfano wa barua rasmi

ISHARA SHULE MSINGI,
S.LP 6015, WATAMU.
26-8- 2007.

MSAJILI MKUU, MAKANI
SHULE YA UPIU, S.LP 21784.
NAIROBI.

**KUH: KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA**

Ni fahari na faraja kwangu kuchukua fursa hii Hi niyatume maombi yangu ya kujiunga na kitado cha kwanza katika shule yako maarufu mwaka huu.

Mimi ni kijana wa kike. Mzalendo kindakindaki wa taifa hili. Nina umri wa miaka kumi na mitano. Nilikuwa katika shule ya msingi ya Ishara. Hapo ndipo nilipoufanyia mtihani wangu wa kutimu na kuhitimu elimu ya msingi mwaka jana.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Katika mtihani wangu huo wa mwaka jana, sina budi kujinadi kwamba, Mwenyezi Mungu zlinijalia nikafaulu na kufuzu vizuri sana. Hayo matokeo yangu bora ndiyo yanayonipa ari na ghera ya kuomba kujiunga na shule murua kama yako. Kwani naelewa na kufahamu dhahiri ihahiri kwamba mwiba uchomeako ndiko utokeako. Nacho kinolewacho hupata. Nao wanoaji 'odari niwapate wapi kama si shuleni pako hapo?

тusiandikie mate ilhali wino upo. Naomba ushuhidie na kuthibitisha ubora wa matokeo yangu <atika nakala niliyoambatisha pamoja na barua hii Hiyo na matokeo kamili yafuatavyo:

- Kiswahili alama 98%
- Kiingereza alama 95%
- Hisabati alama 90%
- Sayansi alama 80%
- Elimu Jamii na Dini alama 85%

Ama kwa hakika hizo ni alama bora ambazo bila tashwishi yoyote zinaweza kunifungulia mlango wa heri na fanaka nikapokelewa kwa mikono miwili katika chuo chako. Kwani kizuri zhajiuza.

Kuhusu maendeleo yangu pamoja na nidhamu, tafadhali uwasiliane na Mwalimu Mkuu wa Ishara. Hapa, aidha, ninaambatisha cheti changu cha kutimu masomo katika shule ya msingi. Kinaonyesha na kutaja maendeleo yangu shuleni, hulka zangu, uraibu na harakati zangu zote tangu awali na aheri katika maisha yangu shuleni. Ni dhahiri kwamba hatuwezi kulifunika jua kwa ungo; napo penye ukweli uongo hujitenga. Naye msema kweli mpenzi wa Mungu.

Natumaini ombi langu litakubaliwa na kupokelewa kwa moyo mkunjufu.

Wako Mwaminifu,

____________________ Latifa Halisawa.

## (c) Insha ya kianzio

Andika insha sanifu isiyo na ila wala kasoro kisarufi ama kimaendelezo itakayoanzia hivi:

GUNIA LA CHUMVI

**Kismati aliporudi aliandamana na polisi wawili. Nilishangaa na kuduwaa. Walinihoji na kunisaili** maswali sufufu...

Naam, mwiba wa kujichoma huambiwi pole. Kismati alikuwa msichana mrembo na mlimbwende. Nilivyomjua Kismati, alikuwa msichana mwenye nidhamu na adabu njema.

Kismati aliniangalia kwa macho ya hasira. Askari mmoja wa polisi alisimama na kusema, "Rafiki yako amepatikana na hatia ya mauaji". Kweli, bahari haishi zingo. Moyo ulinidunda, na kunipapa. Kismati alikuwa mwuaji! Kwa muda wa dakika tano hivi, hakuna aliyeweza kusema wala kukohoa. Kimya! Aha, kimya kingi kina mshindo mkuu.

Kismati alitabasamu na kucheka. Nilimwangalia kwa hasira na ghadhabu, nikamaka "Unatabasamu ilhali uliwauwa wazazi wangu!? Ulijidai ati ulikuwa sahibu yangu! Zuzu wewe!" Nilisema huku machozi yakinitiririka kama maji ya bomba. Waama, gunia la chumvi hurishai chumvi.

**(3031**

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Hisia za uchungu na hasira zilipenya moyoni mwangu. Kismati alikuwa amewaua wazcz wangu. Ama kweli, kizuri hakikosi Ha. NHimwangalia Kismati kwa mara ya pili. Tabasar. ilikuwa imemvaa usoni. Nilipiga unyende, kisha nikajikakamua upesi. Nilimtwanga Kismc. ngumi mgongoni nikamwangusha chini kifudifudi.

Askari polisi alinishika mkono na kunibwaga kwenye kiti. Kismati alisimama polepoler: kusema. "Baradhuli! Wadhani kuwa waweza kunipiga?" NHimwangalia huku mdomo wan:, ukibaki wazi kwa hofu na wahaka. Kwa hakika, hasira hasara. Askari alituangalia kwa maki-Kisha akamwambia Kismati, "Msichana, twende kituoni." Hakika, pwagu hupata pwaguzi.

Askari hao wawili walimvuta Kismati. Baadaye, nilijibwaga sakafuni na kuanza ku,: kwikwikwi. Wazazi wangu walikuwa wameuawa! Mh! Rafiki yangu ndiye aliyekuwa amewau: "Mungu, tafadhali unisaidie!" Nililia kwikwi huku nikipiga unyende. Ni dhahiri shahiri. Munc. kasema niombe nikupe.

Mlango ulibishwa kwa nguvu. Nilisimama nikajikokota kuenda kuufungua. Sahibu yangu w: zamani, Kaimati, alikuwa amesimama kwenye mlango. "Unafanya... nini... hapa?"Nilimwuliz: kwa sauti ya kutetemeka. Kaimati alinijibu, Najua kinachoendelea. Kismati, alikamatwa baac: ya kuwaua wazazi wako. "Nimekuja kukusaidia. Ni wazi kabisa, auguaye huangaliwa. Mir na Kaimati tulikosana baada ya Kismati kuwa rafiki yangu, lakini sasa..." Sikuweza kumaliz: sentensi yangu. Kisha Kaimati akaniambia, "Siela, ya kale hayapo. Tuyagange yajayo ti NHimwangalia Kaimati kwa mshangao, wasiwasi na mashaka. Kumbe, akufaaye kwa dhk ndiye rafiki.

Mimi na Kaimati tulisameheana na tukawa rafiki tena. Baadaye, tulienda zetu kushaurianc Nilimshukuru Mola kwa kunipa rafiki kama Kaimati. Ni kweli, asiyekuridhi mridhi.

## (d) Insha ya Kimalizio/dondoo

Andika insha isiyopungua pande mbili za karatasi ya majibu, ukimalizia hivi: Ashura alishika tama na kumaka, "Lo! Mungu ameninusuru!"

AJALI HAINA KINGA

Machozi yalimchirizika Ashura machoni michirizimichirizi njia nnenne. Mama yake alikuwc amefariki dunia. Alijawa na huzuni, masikitiko na majonzi. Alianza kukumbuka jinsi mama yake alivyokata kamba na kunielezea. Kwani akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Siku moja, Ashura alikuwa amerudi nyumbani mapema. Alipoingia nyumbani, alishangc: na kusangaa kumwona shangazi yake. Alijawa na furaha. Alimsalimia shangazi na kuketi kanc: yake. Walipokuwa wakipiga gumzo, mama yake Ashura aliingia. Alimtuma Ashura dukar Ashura alitoka nyumbani shingo upande na kutembea kwa mwendo wa pole hadi dukan Waama, mwenda pole hajikwai.

Alipofika, alinunua mboga. Alilipa pesa na kuanza safari yake ya kurudi nyumbani. Njian alikutana na rafiki yake Kamri. Walianza kupiga gumzo na kupunga hewa. Watu hawa waw walikuwa masahibu wa chanda na pete yaani, walipendana sana. Kamri alimkaribisha Ashur: nyumbani mwake. Kwa vile Ashura alikuwa amesahau mambo ya mama yake alikubali. Alikuv,: ameisahau na kuitupilia mbali methali isemayo, chelewa chelewa utamkuta mwana si wako.

Takriban saa nane na nusu, Ashura aliamua kurudi nyumbani. Alimwaga rafiki yake na jenda zake. Ashura alipotazama saa yake ndipo alipogundua na kung'amua kuwa amechelewa. 1ikimbia shoti umeme kando, hadi nyumbani kwao akipuuza methali isemayo haraka haraka -aina baraka na pole pole ndio mwendo.

Alifika na kuwasili nyumbani mnamo saa tatu. Umati wa watu ulikuwa umekusanyika rbele ya nyumba yao. Alitunduwaa kwa kiwewe. Aliduwaa na kubung'aa. Nyumba yao ilikuwa <iteketea! Ama kweli, ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni.

Jirani zake Ashura walikuwa wakijaribu juu chini kwa bidii na jitihada kuuzima moto huo. Hapo ndipo alipokumbuka methali isemayo, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Hayawi hayawi huwa. Naam, baada ya saa chache jirani zake walifua dafu kuuzima moto. ^shura aligundua kuwa mama yake amefariki. Waliomfariji Ashura, walimkumbusha kuwa asiye na wake ana Mola. Kwa hakika halahala mtu na jirani.

Binadamu na kifo ni kama nyama na mifupa havifarakani. Yaliyopita si ndwele, tugange yaliyopo na yajayo. Dunia mwendo wa ngisi huzinga mbele na nyuma. Kwa kweli ajali haina kinga. Naam, Ashura alishika tama na kumaka, "Lo! Mungu ameninusuru!"

## (e) Insha ya methali

Andika insha isiyopungua kurasa mbili, kuthibitisha methali ifuatayo.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

ASIYESIKIA LA MKUU HUVUNJIKA GUU

Maana ya methali ni, asiyetii mawaidha ya wakubwa wake hujikuta kwenye taabu. Kweli, ni faradhi tuwatii wakubwa wetu. Chambilecho wahenga, asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

Hapa nilipo sasa, fukara hohehahe, sina mbele wala nyuma. Ninatafakari na kuvuta taswira. Ninatokwa na machozi kupukupu njia mbili mbili ninapokumbuka vile mama alivyokuwa akinionya na kunikanya mara kwa mara kuhusu tabia zangu mbaya za kuwadharau wakubwa wangu. Lakini masikio yangu nikayatia komango. Ama kweli, ukimpigia kiziwi ngoma utapasua kiwambo. Mama alichoshwa na tabia zangu duni. Kumbe, ukumwashia kipofu taa, utayamaliza mafuta.

Siku moja, mimi na sahibu yangu wa kufa kuzikana, Zonge, aliniambia kuwa tuandamane kuenda kutembea. Jua Ulikuwa utosini likitoa miale yake kwa kadiri Mwenyezi Mungu alivyoamuru. Tuliandamana kama nzi mzembe anavyoandama uvundo. Zonge alikuwa na papara na haraka za bure. NHimdokezea kwa sauti nzuri kama kinanda kwamba, haraka haraka haina baraka, kwani mwenda pole hajikwai.

Baada ya hayo, tulitembea asteaste kwa mwendo wa maringo na madaha tukitangatanga na kuzurura hapa na pale kama mbwakoko. Mara tukamwona dalali mnadani akiziweka fulusi zake kibindoni pahali ambapo tungeweza kuzipata. Tulimjongelea nyatunyatu kwa hatua za hesabu huku tukitabasamu kama mamba. Punde, tulizinyakua ngwenje hizo. Lakini, lo! Siku za mwizi zilikuwa ni arubaini tu!

Dalali yule alituona akapiga kamsa na mayowe, "Wezi! Wezi!" Kufumba na kufumbua, kila mtu alitugeukia. Tulipigwa tukapigika ngoma kando. Polisi walikuja na kuokoa maisha yetu dhalili. Niliponea tundu la sindano. Ama kweli, adhabu ya kaburi aijuaye maiti.

Tulifungiwa korokoroni. Tukapelekwa mahakamani. Hatimaye tulihukumiwa kifungo ch: miaka minne. Mimi binafsi, niliona cha mtema kuni. Laiti ningalijua ningaliwatii wakubwa wangi lakini liandikwalo ndilo liwalo na pia yajapo yapokee. Hakika majuto ni mjukuu, huja kinyumt Ninajuta huku nikiamini na kusadiki kwamba asiyesikia la mkuu huvunjika guu.**(f) Insha ya hotuba**

Hotuba ni maelezo yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya hadhira. Hatibu ni anayetoa hotuba. Hadhira ni wasikilizaji.
Utangulizi ni aya ya kwanza ya kutaja waliohudhuria, kujuliana hali na kutaja hatibu na kiini cha hotuba.

## Mambo muhimu katika hotuba

- Hotuba hufaa kuwasilishwa katika kauli halisi au usemi halisi.
- Hotuba hufaa kutangulizwa kwa alama za kunukuu na kufunga kwa alama hizo.
- Ni sharti iwasilishwe katika nafsi ya kwanza.
- Kutambua hadhira ukianza na watu mashuhuri. Kwa mfano:
- Lugha ni lazima iwe fasaha. Uteuzi wa msamiati ufungamane na hotuba yenyewe.
- Hotuba ni sharti ihusishe hadhira. Jambo hili hufanywa kwa kuiuliza hadhira maswali ya balagha.Aidha kuzungumza na kundi baada ya jingine.
- Unapoandika hotuba, usionyeshe mazungumzo ama vitendo vya hadhira.
- Jambo jingine ni kuwa, usiandike hotuba kwa njia ya masimulizi. Hata aya moja.

## Muundo wa hotuba

## Kichwa

- Insha ya hotuba huwa na kichwa ambacho hutokana na mada uliyopewa.
- Anwani ni sharti iafikiane na dhamira ya hotuba pamoja na maudhui.
- Kichwa huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari kwa rula.

## Utangulizi

- Utangulizi wa hotuba huwa rasmi.
- Hatibu huanza kwa kuwataja wageni mashuhuri waliohudhuria kuanzia cheo cha juu kwenda chini. Kisha anatoa salamu.
- Aidha, ni bora kuwataja baadhi ya nyadhifa wanazoshikilia pamoja na majina yao.
- Toa kauli itakayoleta ucheshi ili kuivuta hadhira. (bora tu, kauli hiyo ihusiane na hotuba yenyewe).
- Utangulizi hauna budi kuwa na mnato ambao ni kichocheo cha hadhira kusikiliza.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Taja kiini cha hotuba yako katika utangulizi. Mwili au sehemu kuu

0 Maudhui ya insha hupatikana katika sehemu hii.

- Hoja hupangwa kulingana na uzito wa mawazo.Anza na zile muhimu.
- Ni sharti hoja zipangwe kulingana na utukiaji wake.
- Fafanua hoja zako kwa kulinganisha mambo au kuonyesha tofauti.
- Jadili tatizo na uonyeshe kiini chake. Onyesha athari ya tatizo lenyewe.
- Onyesha suluhisho la tatizo lenyewe.

Lugha

Lugha ni sharti iwe sanifu. Uteuzi wa msamiati uoane na mada na pia uwe wenye mantiki.

- Fani za lugha zitumiwe ili kuifanya insha yenyewe kuvutia. Hitimisho
- Tamati iandikwe kwa kusisitiza mambo muhimu ili kuishawishi hadhira.
- Hitimisho huwa aya moja tu ya mwisho.

## Mifano

## Kielelezo cha kwanza

### HOTUBA YA BURIANI

"Mgeni wa heshima Profesa Majimazuri, mwadhama kasisi, mwenyekiti wa halmashauri ya shule Bi Ahadera, mwalimu mkuu Bwana Nasaha, naibu wa mwali mkuu Bi. Endelea, walimu, wavyele, wanafunzi wenzangu, mabibi na mabwana, shikamoo? Wadogo cheichei? Mimi ni Bongo Timamu, mtahiniwa wa darasa la nane. Nimesimama kidete mithili ya mwiba wa mchongoma Hi niwape mkono wa buriani. Hayawi hayawi, sasa yamekuwa. Safari tuliyoisubiri kwa hamu na pashau sasa imeiva. Safari ya miaka minane si lele mama.

Ninazo nyemi fokofoko, kuwaona namna mlivyofurika furifuri katika uchanjaa huu. Pokeeni mkono wa tahania kwa namna mlivyowasili bila kulimatia. Ama kweli kuwapo kwenu kunaashiria ushirikiano mlio nao. Wahenga waliamba, kinga na kinga ndipo moto uwakapo. Tangu linijifya moja likainjika chungu?

Awali ya yote, ninawashukuru wageni wote waliokubali kuitikia wito wa kuja kujumuika nasi katika hafla hii. Sote tunabaini kuwa, mtu hakatai wito bali aitiwalo.

Kwa walimu, nyinyi mmetufaa kwa dhiki na faraja. Miaka minane ambayo tumekuwa katika shule hii, tunaterema kwa furaha na buraha. Si kwa kuwa bahari yetu ya elimu imekuwa shwari. La! Tulibaini kuwa, nahodha hodari haogopi mawimbi. Zabibu zilipokuwa chungu tulikula katika sahani moja. Na kinyume chake vivyo hivyo. Tunawapigia dua kwa Maulana awape siha njema pamoja na aila zenu.

Kwa wazazi wetu, tunawaambia kongole. Tangu tulipozaliwa, mmetufaa si haba. Si karo, si matibabu, si masurufu. Mmetufaa kwa nasaha, mliepuka kutuengaenga kama yai. Mlitekeleza majukumu yenu ya kuuziba ufa msije mkajenga ukuta. Nyinyi ni johari adimu isiyopatikana popote duniani. Mungu awazidishie neema tumbitumbi. Tutawalipia nini iwe yenu fidia?

Watahiniwa wenzangu, mbiu ya mgambo imepigwa. Aliyelala arauke. Naye aliyezinduka apige mbio. Nyaadhi tumepewa na walimu na wazazi. Mafunzo tumepokea ya kutosha. Nasaha yangu kwenu ni; mfuate maagizo ya mtahini na walimu. Tulifundishwa kuwa, ukitaka kupasi, huna budi kufuata maagizo. Epuka kujifanya mjuvi. Kumbuka kwamba, ajidhaniye amesimama, aangalie asianguke. Sote tujihadhari. Ni bayana kama pengo kuwa, ukicheka na nyani shambani, utavuna mabua.

Fauka ya hayo, mkikamilisha mtihani msisisahau kuwa, dunia ni hadaa ulimwengu shujaa. Kuna mengi mtakayokutana nayo. Jiepusheni na nyendo benibeni. Je, mapenzi miongoni mwenu yana natija gani? Maradhi ya UKIMWI si hadithi za paukwa pakawa. Mihadarati, ujauzito, ubakaji, usagaji, ulawiti, utapeli na ugaidi ni balaa ambazo zitakuletea majuto siku za usoni. Anayebaini usikivu, kumcha Mungu, na kuwaheshimu wazazi, ana baraka mzomzo.

Watahiniwa wenzangu, mwakani tutakuwa, kidato cha kwanza. Kuna mengi tumeyasik : kutama runingani na kusoma katika magazeti. Wanafunzi wanachoma mabweni, kutumia dc~: za kulevya na wanafunzi kula njama kuwaua wanafunzi wenzao. Tusichukue mkondo hut Tumeona wazazi wengi wakilia wanapoona namna watoto wao wanavyofungwa gerezani. Sher I ni msumeno hukata mbele na nyuma. Ukipatikana utakalia kiti moto. Ukanye moyo wak: Fahamu kuwa, mwenye kushiriki moyo asipourudi mtima, hufa maji podoima na kuondoka n:

klcma



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Kwa wanafunzi wanaobaki, fuateni nyayo zetu. Tieni bidii za mchwa wajengao kingulima kwa mate. Jiepusheni na maasi na ugoigoi. Sisi tulipojaribu ujanja, tulizimwa kama kibatari kwa mpulizo mmoja. Waliojaribu kuufuga ujeuri, walikiona cha mtema kuni. Kufaulu katika elimu kunategemea juhudi zako mwenyewe. Pandeni miche yenye natija pekee. Ni nani miongoni mwenu asiyebaini kuwa, ukipanda upepo utavuna tufani?

Pokeeni sifa belele kwa kuhudhuria kikao hiki. Ninaomba radhi iwapo nimeteleza ulimi. Hi msije mkaniita chiriku wanadamu, ninaomba kukomea hapo. Maulana awape mbawazi njema. Asanteni."

## Kielelezo cha pili

**Andika hotuba iliyotolewa na mwalimu mkuu katika mkutano wa wazazi, walimu na wanafunzi** wa darasa la nane.

UMOJA NI NGUZO YA UFANISI

"Mwenyekiti wa halmashauri ya shule Bwana Sossion, naibu wa mwalimu mkuu Bib' Masumbuko, walimu, wavyele na wanafunzi, hamjambo? Kongole kwa kuona namna mlivyofurikc furifuri na kubanana mithili ya mchwa katika kingulima kwenye ukumbi huu. Chambilecho wahenga, mtu hakatai wito bali hukataa aitiwalo. Nimewaita katika mkutano huu Hi tujadiliane kuhusu umuhimu wa elimu katika shule hii iwapo tunahitaji ufanisi. Wahenga waliamba, kambare mkunje angali mbichi.

Tumeafikia maendeleo mengi. Ujenzi wa maktaba umekamilika. Vyoo vilivyosombwa na mvua ya gharika vimekarabatiwa. Fauka ya hayo wanafunzi hawa wetu wameweza kushiriki katika michezo ya kuigiza na tamasha za muziki. Tumeweza kufika ikulu kumtumbuiza rais. Kombe la ushindi tunalo.

Katika upande wa elimu, tulichukua nafasi ya tatu katika jimbo letu. Jambo hili la kutoka nafasi ya kwanza hadi ya tatu tulivyokuwa mwaka juzi linanitia kimuyemuye. Nimelipigia mbizi suala hili na sasa nimeibuka.

Nimeona tuupatilize udongo ungali maji. Kwa hivyo, siwezi kusubiri kuona kitumbua kikiingia mchanga hapo mwakani. Safari ya elimu ina milima na mabonde, misitu na nyika naye msafiri ni aliye Pwani. Azimio la kuwataka wazazi na wanafunzi wa darasa hili la nane, ni kwa kuwa ufanisi unategemea juhudi zetu sote. Walimu, wazazi na wanafunzi. Tangu linijifya moja Ukainjika chungu?

Sote tunabaini kuwa wana wote ni sawa. Hakuna watoto wanaozaliwa wakiwa wala werevL wajinga. Hakuna mtoto anayezaliwa akijua kuongea bali hujifunza. Labda hayawani kamc mbuzi ndio tu hurithi sauti wanapozaliwa. Rabana hana mazoea ya kupendelea. Wahengc walisema, Mungu si Athumani.

Nielezeni dhahiri shahiri ni kwa sababu gani shule fulani nchini ndizo zenye matokeo aula miaka na dahari? Jibu mnalifahamu fika. Wazazi hao hawaengaengi wana wao jinsi Hivyo katika shule hii ya Kayai. Mbona mnainama wazazi? Leo mambo tunayaweka dhahiri. Kwa nini tufunike jua kwa ungo? Ni nani kati yetu asiyebaini kuwa ukimstahi mke ndugu huzai naye? Wazazi kumbukeni, ukicha mwana kulia utalia wewe.

Walimu wetu wapenzi, mna wajibu mkubwa kuwaelekeza vijana wetu. Nyinyi ndinyi rubani katika elimu. Hakikisheni chombo hakizami upande wenu. Palilieni mustakabali wa wanafunzi hawa. Hao ndio taifa la kesho. Chumvi ya taifa.

Wanafunzi, tupeni macho katika janibu zote mwone matumaini. Tieni bidii katika masomo mithili ya mchwa wanaojenga kingulima. Mtaka cha mvunguni sharti ainame. Matokeo bora ya mitihani yanatokana na nidhamu, ari, na bidii. Ninavyojua ni kuwa, ajizi ni nyumba ya njaa. Shime wanagenzi! Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Jiepusheni na mambo yasiyokuwa na natija katika maisha kama mihadarati na mapenzi miongoni mwa wavulana na wasichana. Tumesikia visa vingi vya wanafunzi wakizama katika uraibu wa mihadarati na mwishowe kuangamia katika janga la Ukimwi.

Mimi nina imani na matumaini juu yenu. Fanyeni kama wenzenu wanaofaulu. Msisahau kuwa, ukiona vyaelea jua vimeundwa. Wekeni nadhiri kwa Maulana na sisi sote.

Pokeeni sifa kedekede kwa kunisikiliza. Ninaomba radhi iwapo nimemwudhi yeyote. Binadamu kama kilihali haishi uchafu. Asanteni."

## KCPE

| INSHA ZA HOTUBA KCPE KISWAHILI | | 1993- 2013 |
|---|---|---|
| Mwaka | Aina ya | Insha yenyewe |

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

| | | |
|---|---|---|
| | Insha | |
| 1993 | Hotuba | Wewe ni mmoja wa wanafunzi wanaomaliza masomo katika darasa la nane. Umechaguliwa na wenzako kutoa hotuba ya kuwaaga walimu na wanafunzi wanaobaki shuleni. landike hotuba hiyo. |
| 1997 | Hotuba | Andika insha ya mawaidha yaliyotolewa na mgeni wa heshima siku ya utoaji wa zawadi shuleni mwenu. |
| 2002 | Hotuba | Andika hotuba utakayowatolea wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa usafi wa mwili na mazingira. |
| 2013 | Hotuba | Wewe ni kiranja mkuu katika shule yenu. Umealikwa kuwahutubia wanafunzi wenzako kuhusu umuhimu wa usafi. Andika hotuba hiyo. |

## Mazoezi

1. Wewe ni kiranja wa darasa lako. Umechaguliwa kuwashauri wanafunzi wenzako kuhusu madhara ya mihadarati.Toa hotuba kuwashauri.
2. Andika hotuba ya karamu ya kuwaaga wanafunzi waliomaliza darasa la nane.
3. Hotuba ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwa rafiki yako.
4. Hotuba ya mwanafunzi katika siku ya wazazi shuleni.
5. Hotuba juu ya madhara/athariza mihadarati.
6. Hotuba kuhusu manufaa ya kudumisha usafi wa mwili na mazingira. (g)

## Insha ya mjadala

- Mjadala hutokana na dhana ya kujadili.
- Kujadidli ni hali ya kuzungumzia jambo fulani kwa undani ili kupata wema na ubaya wa kitu, faida na hasara, kufaa na kutofaa, n.k.
- Insha ya mjadala ina sehemu nne muhimu:

### Kichwa

Huandikwa kwa herufi kubwa na hupigiwa mstari. Kichwa chenyewe huonyesha ukinzani wa kimawazo, kwa mfano:

MAISHA YA MJINI NI BORA KULIKO YA SHAMBANI

### Utangulizi

Utangulizi hufafanua mada kwa ujumla. Huangazia kuhusu kinachojadiliwa ili kieleweke barabara.

### Mwili

Mwili wa mjadala huwa na sehemu mbili; sehemu ya kuunga mkono na sehemu ya kupinga mada katika kichwa. Mwanafunzi anatakiwa aanze kujadili upande mmoja kwa kutoa hoja kadha. Kila hoja huandikwa katika aya yake.

Baada ya kumalizia hoja za upande mmoja, anatakiwa ajadili upande wa pili kwa hoja nyingine zinazoonyesha kinyume na hoja za kwanza. Hizi pia huandikwa katika aya kwa kila hoja.

### Hitimisho

Hitimisho huonyesha msimamo wa mwanafunzi katika mjadala. Ni lazima mwanafunzi aonyeshe bayana upande anaosimamia au kuunga mkono. Hakikisha kuwa upande unaounga mkono ni ule uliokuwa na hoja nyingi.

Usiunge mkono mambo mabaya katika jamii. Onyesha msimamo ambao unafaa kuigwa na watu katika jamii kwa kusudi la kuijenga jamii bora.

### Tanbihi

- Andika hoja zako zote kabla ya kuanza kuandika mjadala. Ukifanya hivyo hutakanganyikiwa katika utiririko wa mawazo ukianza kuandika.
- Jadili hoja kuu kadri iwezekanavyo

TEKNOLOJIA MPYA IMELETA HASARA NA FAIDA

Teknolojia mpya ni matumizi ya vifaa au mashine katika kuboresha maisha na taaluma mbalimbali katika maisha yetu. Vyombo kama vile runinga, tarakilishi na taaluma kama mtandao wa intaneti, ni maarifa katika teknolojia mpya.

Teknolojia mpya imawaharibu vijana kimaadili. Vijana wameiga mambo mabaya katika sinema na katika tamaduni potovu za kigeni. Mathalani, mitindo ya mavazi ambayo haina heshima. Kuiga lugha chafu kutoka kwa wanamuziki wa kimagharibi. Kutazama filamu za ngono na makala ya kupotosha. Kutazama vilamu za vita ambazo zimesababisha vijana kutokwa nc utu. Maadili yamepotea.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Uhalifu umezidishwa na teknolojia mpya. Magenge ya wahalifu yamezua mbinu mbalimbali z: kutekeleza uhalifu kwa kutumia mtandao na simutamba. Jamii zetu si salama tena. Matapeli - imekuwa wakitumia watu arafa na kuwarubuni fedha zao. Fauka ya hayo, rununu na mitandao ■ metumika katika mipango ya utekaji nyara. Aidha ugaidi umefanikishwa na matumizi ya -.zKnolojia kwa kutega guruneti na kulipua kwa kutumia rununu.

Kwa upande mwingine, teknolojia mpya imewasaidia wananchi kupata taarifa zinapochipuka <ila mahali duniani. Ni vifaa muhimu vya kusambaza habari kama vile runinga na redio. Iwapo unafanya utafiti katika nyanja mbalimbali ni rahisi kupata mitandaoni.

Teknolojia mpya ni chemchemi ya ajira. Watu wengi wameweza kuajiriwa katika vituo vya runinga, redio na mtandao. Wengine wameanzisha biashara zao wenyewe kwa kutoa huduma ama kuuza rununu, runinga, kukarabati tarakilishi, kutia ujumbe katika kompyuta. Wanachuma riziki kutumia teknolojia hii mpya.

Sekta ya biashara. Kwa kutumia teknolojia mpya, bidhaa nyingi zimeweza kuuzwa na kuwafikia wasiokuwa nazo. Matangazo ya biashara hupeperushwa katika vyombo vya habari na watu hufaidi kupata bidhaa muhimu. Ni rahisi kuweza kununua bidhaa hata mahali ulipo bila kusafiri. Pia ni rahisi kujua bidhaa mpya sokoni.

Licha ya teknolojia mpya kuwa na hasara zake, faida zake ni nyingi hata zaidi. Matumizi ya teknolojia mpya yataifaa jamii lakini wananchi wasiitumie vibaya.

## Mazoezi

1. Ajira za watoto zimeleta madhara makubwa katika jamii. Jadili.
2. Ukabila umechochea vita sana nchini. Jadili.
3. Shule za mijini ni bora kuliko za mashambani. Jadili.
4. Ubaguzi wa jinsia umechangia dhuluma za kijinsia. Jadili.
5. Tohara ya jinsia ya kike imechangia pakubwa kumdhalilisha mwanamke. Jadili.

### (h) Insha ya mazungumzo

Mambo muhimu

- Kichwa kinachoeleza wazungumzaji
- Utangulizi wa mazungumzo kwa kifupi
- Kuna sehemu ya wazungumzaji na ya semi zao.Tenga barabara.
- Maelezo yoyote huwekwa katika mabano (Epuka 'na' ya wakati. Badala yake tumia 'ki')
- Majina yote yawe ya Waswahili.
- Mada za mazungumzo huenda zikabadilikabadilika.
- Zingatia urefu wa insha kulingana na maagizo.

MAZUNGUMZO BAINA YA ANITA NA AMALI

(Anita na Amali walisoma pamoja katika shule ya upili miaka ishirini iliyopita. Wamepatana hotelini kwa chakula cha mchana. Wameketi wakiangaliana ana kwa ana.)

Anita: Nimeshukuru sana kukuona! Amali:

Nimeshukuru pia! Karibu sana Anita.



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Anita: Mmmh! Nieleze kuhusu maisha yako kwa kifupi.

Amali: (Akitabasamu)Mmh! Mimi kwa sasa ni mkurugenzi wa kampuni moja ya saruji humu jijini Baraka. Ninaishi na familia yangu ya watoto watatu. Mume wangu naye ni mhandisi wa serikali. Ninashukuru kwa baraka zake Mola!

Anita: (Akionyesha kufurahishwa).Sadakta! Una maisha mema si haba!

Amali: (Kwa kicheko hafifu)Yoteni ya Mola. Sisi ni kama tu vyombo. Je, wewe?

Anita: (Akikohoa kwanza)Mimi nimekuwa mfanyikazi wa serikali kwa miaka kumi. Kwa sasa mimi ni daktari katika hospitali ya Ponea. Nimeolewa na nina watoto wawili. Mume wangu ni kanali katika jeshi la taifa.Tunaishi katika mtaa wa Buraha.

(Endeleza mazungumzo haya...) (i)

## Insha za dondoo

Dondoo ni nukuu iliyotolewa kutoka katika maandishi ama mazungumzo fulani.

- Dondoo ni aina ya insha ambayo mwandishi hupewa maneno ya mwanzo kisha hutakiwa kuimalizia insha yenyewe.
- Aidha, mtahiniwa anaweza kupewa tamati kisha abuni insha.
- Katika insha hii, mtahiniwa hana budi kuyafasili maneno aliyopewa ili asipotoke.
- Ubunifu wa matukio ni muhimu sana.
- Ni sharti mwandishi ajenge mgogoro katika insha yake. Kumbuka, mgogoro si jambo la huzuni ama mashambulizi kama watahiniwa wengi wanavyodhani.
- Lugha atakayoitumia mtahiniwa inafaa isheheni maadili.
- Insha ya mtahiniwa ni sharti iwe na mtiririko na mshikamano bora wa mawazo.
- Muundo wa insha za dondoo
- Anwani /kichwa au mada
- Insha ya dondoo sharti iwe na kichwa.
- Anwani hutokana na dondoo au insha utakayoiandika.
- Mada huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari. Iwapo umepewa mfano kama huu:

  Mvua ambayo haikutarajiwa ilianza kunyesha bila kupusa (endelea)

  Basi anwani inaweza kuwa:

- Mvua ya mpepea
- Mvua ya gharika
- Mafuriko
- Mvua ya kifuku
- Mvua ya masika

## Utangulizi

- Insha ya dondoo huwa na utangulizi.
- Utangulizi hutokana na dondoo lenyewe.
- Utangulizi uwe mfupi wa aya moja pekee.

## Mwili au sehemu kuu

- Sehemu hii, ndiyo insha yenyewe. Maudhui huwa yamejadiliwa katika kila aya.
- Mtahiniwa sharti aandike matukio kwa mtiririko murua.
- Ujumbe kwenye aya unafaa uwe bayana.
- Mtahiniwa anafaa abuni ucheshi, mvuto na kujenga mgogoro na taharuki.

## Mpango na mtindo

- Insha ya dondoo huwa na mpangilio wa aya kutoka mwanzo hadi hitimisho.
- Mtindo ambao hutumika ni wa kisimulizi.
- Matumizi ya nyakati hutegemea matukio ya mtahiniwa.

## Lugha



Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

- Lugha itakayotumiwa iwe sanifu na yenye maadili.
- Aidha, ni sharti lugha ioane na fasili ya dondoo lenyewe.

## Msamiati na fani za lugha

Matumizi ya msamiati hutegemea mada aliyopewa mtahiniwa.
Mtahiniwa hana budi kutumia fani za lugha katika kazi yake. Iwapo hatatumia, basi insha itakuwa chapwa. Fani hizo lazima zilenge mada moja kwa moja.

## Tamati ama Hitimisho

- Hitimisho la insha ya dondoo hutokana na mwanzo, utangulizi na mwili wa insha yenyewe.
- Tamati iwe na uhusiano wa moja kwa moja na insha yenyewe.
- Mtahiniwa stadi huhitimisha kazi yake kwa mnato na hasa mwisho ambao hatarajiwi.

## Mifano ya insha za dondoo

## Kielelezo cha kwanza

Anza hivi:

**Yalikuwa majira ya mafungia nyama. Nilikuwa nimetoka shuleni mapema kama ilivyokuwa** ada yangu...

BURIANI PONO NA FOFO

Yalikuwa majira ya mafungia nyama. Nilikuwa nimetoka shuleni mapema kama ilivyokuwa ada yangu. Mimi na umbu zangu Pono na Fofo tulimsaidia nina kutayarisha chajio. Usiku mchanga tulikuwa tumeandika meza kwa kilalio kilichokuwa kitamu mithili ya halua. Baada ya kushtaki njaa, ndugu yangu mnuna alipiga bismillahi. Kisha kila mmoja akaingia katika malazi yake. Muda si muda, bahari ya jumba letu ilitawaliwa na mikoromo. Kila mmoja alikuwa amelala kigogo.

Usiku wa manane, njozi niliyoota ilikatizwa ghafla na joto jingi. Joto hilo liliandamana na harufu ya mchanganyiko wa vitu vilivyokuwa vikiungua. Moshi ulinichonyota kooni. Kupumua kukawa muhali. Nilianza kukohoa mithili ya mwele wa kifua kikuu.Bila kulimatia.niliyapiga mablanketi teke yakadakwa na mfumbati wa kitanda cha ndugu yangu mwanambee aliyelala sako kwa bako na kitanda changu cha mwakisu.

Niliupiga mlango wa chamba chetu teke, nao ukasalimu amri. Nikatoka shoti huku nikipiga usiahi, 'Moto! Moto!' Wavyele nao walitokeza huku wakipiga kamsa. Tukawa tukijimbizana nyange kama mashairi ya ngonjera. Wakati huo, mama alikuwa amemweleka mziwanda wetu mgongoni.

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211

Powered by: -iToschool- | www.schoolporto.com | System developed by: lule 0752697211